# “Upendo wa Mwenyezi Mungu kwa Waislamu”

## *‘Taurati na Injili … uongozi kwa watu!*

BISMILA-HIR RAHMA-NIR RAHIM

بسم الله الرحمن الرحيم

Assalamu’ Aleikum!

Amani ya Mwenyezi Mungu na iwe juu yako na apate kukuongoza katika maisha yako.

Kurani Tukufu yatuambia kwa nini tusome Taurati na Injili (ya Maandiko ya Biblia). Katika Sura 3:3 yatuambia haya: ‘Amekuteremshia (hatua kwa hatua) Kitabu kwa haki, kinachosadikisha yaliyokuwa kabla yake. Na aliteremsha Taurati (Sheria ya Musa) na Injili (ya Yesu) zamani - ziwe uongozi kwa watu, Na akateremsha vitabu vingine vya kupambanua (baina ya haki na batili).’

Inaeleza wazi kabisa ya kwamba Taurati (Sheria) na Injili vilitolewa kwa ajili ya watu wote… “ziwe uongozi kwa watu”.

Twafundishwa katika Kurani Tukufu Sana kwamba kwa njia ya Masihi Isa (Kristo Masihi) hiyo Injili iliteremshwa kuwa ‘uongozi’ na kuwa ‘mauidha’ kwa wamchao (Mwenyezi Mungu). Sura 5:46

‘Na tukawafuatishia (Mitume hao) Isa bin Maryamu kuyahakikisha yaliyokuwa kabla yake katika Taurati (Sheria), na tukampa Injili iliyomo ndani yake uongozi na nuru na isadikishayo yaliyokuwa kabla yake katika Taurati, na uongozi na mauidha kwa wamchao (Mwenyezi Mungu).’ 005:046 Al Maidah.

Mauidha haya (Taurati na Injili) ni onyo, au karipio dhidi ya makosa, yanatushauri tusijiingize katika matendo mabaya. Watu wenye akili timamu, ambao sikio lao liko tayari kupokea mafundisho ya Mwenyezi Mungu, daima watatii maonyo yatokayo Mbinguni, kama vile alivyofanya Musa katika (Injili) Waebrania 8:5. Mwenyezi Mungu ameyalinda kwa makini Maneno yake kama ilivyoandikwa katika Sura 5:48. “Na tumekuteremshia Kitabu kwa (ajili ya kubainisha) haki, kinachosadikisha vitabu vilivyokuwa kabla yake, na kuvihukumia …. Ni faraja iliyoje kujua kwamba Mwenyezi Mungu anayalinda Maneno yake na kuyahukumia, ili sisi leo tupate kuwa na uongozi hakika kuhusu yale yaliyo ya haki na yaliyo batili.

### Je! Taurati na Injili vimechauia?

Watu wenye makusudi mazuri watakuambia kwamba vitabu hivi vimechafuliwa! Fikiria kusema mambo kama hayo juu ya Vitabu hivi Vitakatifu vilivyoteremshwa kutoka kwa Mwenyezi Mungu? Ni kufuru kwake! Kana kwamba Mungu Mwenyezi hawezi kuyalinda maneno yake mbali na watu wenye mawazo mabaya! Lakini kutoka kwa watu hao hao wasemao kwamba Vitabu hivi Vitakatifu vya Taurati na Injili vimebadilishwa au kuchafuliwa utaona wananukuu kwa wingi kutoka katika vitabu hivyo kuendeleza fikara zao! Hata wanakariri sehemu kubwa za Maandiko ya Biblia na halafu wanasema yamechafuliwa, tena watakuambia kuwa haya si Maneno yake Mwenyezi Mungu! Enyi rafiki kama hivyo ndivyo mambo yalivyo, kwa nini myajaze mawazo yenu na vitabu ambavyo vimechafuliwa? Nyakati zingine wananukuu kwa wingi kutoka katika vitabu hivi vinavyodhaniwa vimechafuliwa ili kuthibitisha wazo lao, lakini wanawezaje kuwa na hakika kwamba kile wanachonukuu hakijachafuliwa? Mawazo ya watu hao yameshawishiwa sana na Ibilisi (Shetani). Mungu Mwenyezi ajua fika alifanyalo! Hebu na tumwamini na kutulia juu ya Maneno yaliyoteremshwa kutoka kwake na kuyatwaa maneno haya na kuyafanya yawe yetu wenyewe. Mpendwa wangu msomaji, je, unamcha Mwenyezi Mungu? Basi maneno haya yameandikwa kwa ajili yako wewe!

### *Mawe ya Umbali…*

Siku hizi watu wanahitaji kuelekezwa. Mara ngapi watu wanaosafiri katika njia kuu nyingi wanaangalia Mawe ya umbali barabarani kujua njia ipi na umbali gani kwenda kwenye mji walioukusudia. Katika ulimwengu huu, sisi sote tunahitaji mawe ya umbali kutuambia njia ipi tusafiri salama ili tuweze kufika Mbinguni tuendako. Vitabu hivi Vitakatifu (Maandiko) ni mawe ya umbali (miongozo) ambayo yatakusaidia, na kukufanya usipotee njiani. Lakini leo watu wengi mno wanasafiri katika maisha wala hawatambui kwamba wamo katika barabara kuu iliyokosewa.

Kurani Tukufu yatuambia ‘mwaminini Mwenyezi Mungu na Mtume wake … na Vitabu alivyoviteremsha zamani.’ Sura 4:136. Kwa maana wale wote wanaowakanusha “Mitume wake… Vitabu vyake” wamepotea na kwenda mbali sana.

Watu wameukataa uongozi na nuru, iliyoteremshwa, na wamechagua badala yake kubaki katika giza la ulimwengu huu. Ibilisi (Shetani) amepofusha macho yao kweli, lakini Mwenyezi Mungu kwa anatuita tuje kwenye nuru tukufu ipatikanayo katika Maandiko (Biblia).

“Huu ni ukweli uliotoka kwa Mola wenu” Sura 18:29. Ni kwa njia ya ule ukweli Mwenyezi Mungu anawatakasa watu wake. Injili, Yohana 17:17 – “Uwatakase kwa ile kweli; neno lako ndiyo kweli.” Neno lake Mwenyezi Mungu ndiyo kweli.

Mwenyezi Mungu ni mwenye hekima tosha na mwenye uwezo tosha kuweza kuhukumia na kuyalinda Maneno yake. Sura 6:115 – “Na yametimia maneno ya Mola wako kwa kweli na uadilifu. Hakuna awezaye kuyabadilisha maneno Yake. Na Yeye ndiye asikiaye (na) ajuaye.”

Katika “Injili iliyomo ndani yake [umo] uongozi na nuru na isadikishayo yaliyokuwa kabla yake katika Taurati”. Sura 5:46

Kwa hakika hata Mtume Muhammad aliyewatia moyo Waislamu kusoma Injili alijua yale yaliyokuwamo ndani ya hiyo Injili, kwa maana angewezaje kusema kwamba ilikuwa uongozi na nuru kama yeye alikuwa hajui yale yaliyokuwa yameandikwa mle.

Endapo Mtume Muhammad asingetaka sisi tuisome Injili au Taurati, basi, asingekuwa amesema maneno yenye nguvu kama hayo kusadikisha kwamba Injili na Taurati ni uongozi kwetu leo. Kwa maana yeye alisema viwe uongozi kwa “wale wamchao Mwenyezi Mungu”. Sura 5:46. Rafiki zangu, mkimcha Mwenyezi Mungu, basi, ninyi pia mtatumia muda wenu fulani kuyasoma Maandiko ya Biblia.

Ni katika Maandiko ya Biblia, kama Kurani Tukufu isemavyo, twaweza

“Kupambanua” baina ya haki na batili (Sura 3:3-4). Kamusi yatuambia kwamba “Kupambanua” ni ‘kanuni’ ambayo mambo yote yapaswa kupimwa kwayo kama ni ya haki au batili. Wote watahukumiwa kwa kanuni hii, kwa maana Nabii Isaya (Taurati) alisema katika sura ya 8:20 – “Na waende kwa Sheria (Taurati) na Ushuhuda; ikiwa hawasemi sawasawa na neno hili, bila shaka kwa hao hapana asubuhi.” Kwa Sheria, hii inahusu ile Sheria ya Amri Kumi, na kwa Ushuhuda, ni ushuhuda wa Maandiko. Katika Injili, Masihi Isa anatufunulia sisi jinsi itupasavyo kuishi. ‘Mtu hataishi kwa mkate tu, ila kwa kila neno litokalo katika kinywa cha [Mwenyezi] Mungu .” Mathayo 4:4

### *Taa na Mwanga…*

Sura 17:55, inasema kwamba mitume wengine walipewa vipawa, na kwa Daudi alipewa kipawa cha Zaburi. Katika Zaburi inasema hivi kuhusu Neno la Mwenyezi Mungu,

"Neno lako ni taa ya miguu yangu, na Mwanga wa njia yangu" Zaburi 119:105. Hivi umejaribu kutembea katika giza la usiku bila mwanga? Je, uliona vigumu kabisa kutembea pasipo kuwa na hofu ya kuanguka chini au kukanyaga mahali fulani ambapo ungejeruhiwa au hata vibaya zaidi kuanguka chini ya genge refu?

Watu wengi sana wamepotea mbali sana kutoka kwenye njia ya haki, wameitupilia mbali "Taa" na "Mwanga" ambao kwa huo twaweza kuijua njia sahihi. Kwa nini siku hizi kuna uhalifu mwingi sana, uasi, mmomonyoko wa maadili? Kwa nini jamii iko ukingoni mwa maangamizi? Je, hawajamkana Mwenyezi Mungu, Sheria [Taurati] yake, Vitabu Vyake na mitume wake? Sura 4:136. Hivyo, basi, kila mmoja, haidhuru wewe uwe nani, anasisitiziwa kusoma "Maandiko ya Biblia" ambayo yameteremshwa kwetu kutoka Mbinguni. Hayo kwa hakika yamekuwa ndiyo "kanuni" kwa ajili yetu. Kutufundisha sisi yaliyo ya haki na yaliyo haramu.

(Taurati) Yeremia 29:13 - 'Nanyi mtanitafuta na kuniona, mtakaponitafuta kwa moyo wenu wote.' Wale wamtafutao Mwenyezi Mungu yawapasa kumtafuta kwa moyo wao wote.

## 'Habari Njema kutoka kwa Mwenyezi Mungu'!

Kwa kweli hata Neno moja tu kutoka kwa Mwenyezi Mungu lingekuwa Habari Njema! Watu wangepaswa kushukuru jinsi gani kupokea kitu cho chote kutoka kwa Mwenyezi Mungu! Tunaambiwa katika Kurani Tukufu kwamba alituteremshia sisi huyo 'Neno' na jina lake alikuwa ni Kristo Yesu (Masihi Isa). Sura 3:45: '(Kumbukeni) waliposema Malaika: "Ewe Maryamu! Mwenyezi Mungu anakupa habari njema za (kumzaa mtoto bila ya mume, bali kwa kutamkwa) Neno tu litokalo kwake la kukwambia 'Zaa' ukazaa pasina kuingiliwa). Jina lake ni Masihi, Isa, mwana wa Maryamu, mwenye heshima katika dunia na Ahera, na miongoni mwa waliopelekwa mbele na Mwenyezi Mungu." Hizi ni "Habari Njema" kweli kweli!

Mwenyezi Mungu alichagua kumteremsha mmoja anayeheshimiwa na aliye karibu sana naye. Sura 3:45. Kwa hakika kabisa Kurani Tukufu haiwezi kukosea.

Katika Sura 5:46 twaambiwa kwamba Yesu (Masihi Isa) aliteremshwa kutoka kwa Mwenyezi Mungu kuihakikisha Sheria na Injili (Taurati na Injili), ambamo ndani yake umo Uongozi na Nuru. Siyo tu inatuambia sisi kwamba Taurati na Injili vilihakikishwa, bali pia inatuambia katika Sura 5:48 kwamba hayo Maandiko (Biblia ) yali"lindwa". Hivyo Nabii Muhammad alikuwa akiwaelekeza wale walioitafuta kweli katika Neno lililotoka kwa Mwenyezi Mungu. Kwenye Uongozi huo na Nuru hiyo tunamwelekeza msomaji, yaani, kwenye Injili ambayo katika Waebrania 1:3 inasema kwamba Masihi Isa (Kristo Masihi) "ni … chapa ya nafsi Yake [Mwenyezi Mungu], akivichukua vyote kwa amri ya uweza wake, … aliketi mkono wa kuume wa Ukuu huko juu."

### *Karibu sana na Mungu Mwenyezi!*

Masihi Isa (Kristo Masihi) baada ya kuwa hapa duniani, aliketi mkono wa kuume wa [Mwenyezi] Mungu, na yuko 'karibu sana na Mwenyezi Mungu'. Sura 3:45

Kwa vile sisi tu wenye dhambi, hatuwezi kumwona Mwenyezi Mungu na kuwa hai, bado tunahitaji kumjua Mwenyezi Mungu. Katika Injili, Yohana 1:18, tunaambiwa kwamba 'Hakuna mtu aliyemwona Mungu wakati wo wote' … ni Kristo (Masihi Isa) pekee … 'aliye katika kifua cha Baba, huyu ndiye aliyemfunua.' Wanadamu hawawezi kumtazama Mwenyezi Mungu na kuwa hai, hata hivyo Mwenyezi Mungu kwa Rehema zake alimteremsha Mmoja aliyekuwa "katika kifua" chake na ambaye yuko karibu sana naye, kuwa "chapa" ya Mwenyezi Mungu.

Katika maisha ya Masihi Isa tunaona Upole na Huruma za Pendo lake Mwenyezi Mungu linalodhihirishwa kwa ukamilifu kabisa kwa wanadamu. Maneno ya Isa katika Injili ni haya … "Aliyeniona mimi amemwona Baba" (Yohana 14:9). Sasa twaweza kuwa na picha bora zaidi kuhusu vile alivyo Mwenyezi Mungu, ambayo imejengwa juu ya maisha yake Masihi Isa.

Je! kuna ajabu yo yote kwamba Kurani Tukufu Sana inazo zaidi ya aya 90 zisemazo wazi kabisa juu ya Isa (Kristo Masihi). Sura kumi na tano katika Kurani Tukufu hunena habari zake Yeye. Nabii Muhammad alijua fika umuhimu wa kumwelewa Masihi Isa kuwa ni nani, vinginevyo asingekuwa amenena habari zake katika Sura nyingi sana za Kurani Tukufu. Sisi tungebarikiwa sana endapo tungetumia muda wetu kumfahamu Mtu huyu mashuhuri sana kama kumbukumbu zake zilivyoandikwa katika Injili.

Katika Injili ya Maandiko ya Biblia, twasoma jinsi Masihi Isa alivyokwenda huku na huku akiponya magonjwa na maradhi ya kila namna, wanaume, wanawake, watoto hata na wale wenye ukoma waliponywa na kuwa wazima. Mara nyingi walemavu waliponywa na wafu wakawa hai. Ni furaha iliyoje hiyo iliyoletwa na mambo hayo miongoni mwa watu! Masihi Isa alipotembea katika njia zenye vumbi toka kijiji kimoja hadi kijiji kingine, huruma yake ilijidhihirisha waziwazi. Alikuja kumfunua alivyo hasa Mwenyezi Mungu. Ndani yake Masihi Isa (Kristo Yesu) twaona picha yake Mwenyezi Mungu ambayo kabla yake ilikuwa haijapata kufunuliwa kamwe kwa kina kama hicho.

Kurani Tukufu yaendelea kutuambia sisi kwamba wale wamfuatao Kristo (Masihi Isa), Mwenyezi Mungu a'tawaweka wale waliokufuata, juu ya wale waliokufuru.' Sura 3:55. Rafiki zangu, je, si jambo la maana, basi, kufanya uchunguzi juu ya maisha ya Mtu huyu aliyeteremshwa na Mwenyezi Mungu? Ikiwa Nabii Muhammad alisema juu ya wale wamfuatao Masihi Isa kuwa wangewekwa juu ya wale wanaokufuru, basi, ni halali kabisa kwetu kujua habari zake huyo Isa (Kristo Yesu) na pia kuwa wafuasi wake.

Kwa kutuhakikishia, Kurani Tukufu inatuambia kwamba wale walio wanafunzi wa (yaani, wamfuatao) Isa (Kristo Masihi), yaani wasaidizi hao wa Mwenyezi Mungu, wangepaswa kuitwa kuwa 'wamejisalimisha' kwake. Sura 3:52

Sisi sote twajua kwamba "Mwislamu' ni mtu aliyejisalimisha na kumtii Mwenyezi Mungu. Utii huu hauna swali wala haubakizi kitu kwa upande wetu. Utii huu ni lazima utolewe pia kwa yule Neno (Masihi Isa) aliyeteremshwa kuja kwetu kutoka kwa Mwenyezi Mungu. Kumbuka Sura 3:45 isemayo kwamba Mwenyezi Mungu "anakupa … Neno tu litokalo kwake … Jina lake ni Masihi, Isa," Kwa maana Mwenyezi Mungu, Aliye Mtakatifu, asingefanya mambo yote hayo yaliyo ya lazima kumteremsha Neno wake kuja kwetu katika maisha ya Masihi Isa kama jambo hilo lisingekuwa la maana.

Hebu sikiliza, ewe rafiki yake Mwenyezi Mungu, ametuteremshia Neno wake kweli kweli kuja kwetu, katika umbile la Masihi Isa (Kristo Yesu). Asingekuwa mtu ye yote tu bali ni yule Neno (Masihi Isa) ambaye yu karibu na Mwenyezi Mungu kuliko wote, naye anatoka katika "kifua" cha Baba. Mtu huyo wa maana sana, atokaye katika kifua cha Mwenyezi Mungu, hatuna budi kumjali kwa njia ya pekee, vinginevyo, tutaonekana kuwa tunamtolea matusi makubwa sana Mwenyezi Mungu.

Masihi Isa alipokuwa kando ya mto Yordani ili kubatizwa na kuwa kielelezo kwetu, Maandiko yatwaambia kwamba mbingu zikamfunukia na sauti yake Mungu ikasikika … (Injili) Mathayo 17:5 'Alipokuwa katika kusema, tazama, wingu jeupe likawatia uvuli; na tazama, sauti ikatoka katika lile wingu, ikasema, Huyu ni Mwanangu, mpendwa wangu, ninayependezwa naye; msikieni yeye.' Maneno hayo mawili ya mwisho, 'msikieni yeye' ni ya muhimu kwetu kwamba tusikilize yale ambayo Mwenyezi Mungu ametuteremshia ndani ya Masihi Isa!

Injili, ambayo Muhammad alituambia kwamba iliteremshwa kutoka kwa Mwenyezi Mungu, Sura 3:3, ina aya za Maandiko ambazo zinarudia kusema baadhi ya mawazo yale yale yapatikanayo katika Sura 3:45 ambayo hunena juu ya Masihi Isa kuwa ndiye 'Neno aliyeteremshwa kutoka kwa Mwenyezi Mungu'. Injili Yohana 1:1 'Hapo mwanzo

kulikuwako Neno, naye Neno alikuwako kwa [Mwenyezi] Mungu, naye Neno alikuwa Mungu.' Kisha inaendelea kutuambia sisi kwamba "Naye Neno alifanyika mwili, akakaa [akateremshwa] kwetu" aya ya 14. Ni huyu Neno aliyetuonesha sisi Mwenyezi Mungu alivyo hasa.

Huyu si mwana aliyezaliwa kimwili kama watu leo walivyo na watoto. Lakini huyu ni yule Mmoja aliyezaliwa na bikira, ambaye alikuwa bado hajamjua mume. Kumbuka kwamba hakuna neno lo lote lililo gumu kwa Mwenyezi Mungu! Yeye aweza kusema tu na mambo yakawa vile. Soma tena Sura 3:46

### *Je! huyo ni Mwanawe (Mwenyezi) Mungu?*

Usikate tamaa unaposikia kifungu hiki cha maneno "Kristo, Mwana wa Mungu" hii haimanishi kwamba [Mwenyezi] Mungu anaye mwana aliyemzaa kwa njia ile ile wanadamu wanavyozaa watoto, kwa maana hilo kamwe haliwezi kuwa hivyo. Lakini kinamtaja Kristo kuwa ni Mwana kwa maana ile ambayo Isa yuko karibu sana na Mwenyezi Mungu na ni kwa njia ya Isa (Kristo) tabia ya Mwenyezi Mungu inadhihirishwa vizuri sana kwetu. Njia iliyo wazi kabisa na bora kabisa kwa Mwenyezi Mungu kuwasiliana na wanadamu ni kumtumia mmoja anayefanana na sisi! Hivyo Yeye ndiye Neno kutoka kwa Mwenyezi Mungu …"msikieni yeye".

### *Kichaka Kilichowaka Moto*

Mpendwa rafiki usifikiri hata kwa dakika moja kwamba Mwenyezi Mungu amewekewa mipaka na hawezi kufanya hili. Kumbuka kisa cha Musa na kichaka kilichowaka moto. Kinatuambia kwamba Mwenyezi Mungu alinena na Musa kutoka katika ule moto. Kama Mwenyezi Mungu anaweza kuja kwa mfano wa kichaka kinachowaka moto, je! hawezi pia kuja katika umbile la Mwanadamu na kujidhihirisha Mwenyewe kwetu na kunena nasi? Hakuna kitu cho chote kilicho kigumu kwa Mwenyezi Mungu!

Mwenyezi Mungu na akubariki sana unapotafuta kufanya mapenzi yake na kuchagua kutii kile alichokudhihirishia wewe. Neno kutoka kwa Mwenyezi Mungu ndani ya Kristo Masihi hizo kwetu ni "Habari Njema" 'msikieni yeye'!

Kabla hujafungua kurasa za Vitabu Vitakatifu, daima omba Mwenyezi Mungu akufundishe kuwa na ufahamu sahihi usomapo. Mwenyezi Mungu anawabariki wale wanaojifunza kwa unyofu wa moyo na wanaoitafuta haki. Yeremia 29:13 'Nanyi mtanitafuta, na kuniona, mtakaponitafuta kwa moyo wenu wote.' Wale wamtafutao Mwenyezi Mungu, hawana budi kumtafuta kwa moyo wao wote.

### *Al-Baqara 002.153*

'Enyi mlioamini! Jisaidieni (katika mambo yenu) kwa subira na Sala; bila ya shaka Mwenyezi Mungu yu pamoja na wanaosubiri.'

## "Ibrahimu, Rafiki [Khalil] yake Mwenyezi Mungu"

### *Khalil (Msiri) wa Mwenyezi Mungu!*

Mpendwa msomaji, hebu fikiria tu kule kuitwa "rafiki" [Khalil] yake Mwenyezi Mungu! Je, waweza kupiga picha ya kitu cho chote kilicho cha maana katika ulimwengu huu kuliko hicho? Hakuna cho chote ambacho kingeleta tumaini zaidi kwa mtu kuliko kuitwa "Rafiki yake [Khalil] Mwenyezi Mungu!"

004:125 'Na nani aliye bora kwa dini kuliko yule ambaye ameuelekeza uso wake kwa Mwenyezi Mungu, naye ni mwema, na anafuata mila ya Ibrahimu (kuwa Mwislamu kweli kweli). Na Mwenyezi Mungu amemfanya Ibrahimu kuwa kipenzi chake.' Sura: 004:125 An Nisaa

Kumbuka kwamba Musa aliteremshiwa Sheria (Taurati). Sura 5:44 "Hakika tuliteremsha Taurati yenye uongozi na nuru… Na wasiohukumu kwa yale aliyoteremsha Mwenyezi Mungu, basi hao ndio makafiri." Sura: 005:044 Al Maidah

Tafadhali zingatia haya. Taurati 2 Mambo ya Nyakati 20:7 "Si wewe, Ee [Mwenyezi] Mungu wetu, uliyewafukuza wenyeji wa nchi hii mbele ya watu wako Israeli, ukawapa wazao wa Ibrahimu rafiki yako [Khalil] hata milele?'

Ni heshima iliyoje kuwa rafiki wa karibu sana wa Mwenyezi Mungu! Twaweza kujifunza zaidi juu ya kuwa rafiki zake Mwenyezi Mungu katika Injili. Sura 5:46 "Na tukawafuatishia (Mitume hiyo) Isa bin Maryamu kuyahakikisha yaliyokuwa kabla yake katika Taurati, na tukampa Injili iliyomo ndani yake uongozi na nuru na isadikishayo yaliyokuwa kabla yake katika Taurati, na uongozi na mauidha kwa wamchao (wanaomwogopa)." 005:046 Al Maidah. Twaigeukia (Injili) Yakobo 2:23 "Maandiko yale yakatimizwa yaliyonena, Ibrahimu alimwamini [Mwenyezi] Mungu ikahesabiwa kwake kuwa ni haki; naye aliitwa Rafiki [Khalil] wa [Mwenyezi] Mungu."

### *'Marafiki Zake' Wengine wa Mwenyezi Mungu!'*

Musa alipata majaribu makubwa ya imani katika maisha yake. Hata hivyo, yeye aliendelea kuwa mwaminifu kwa Mwenyezi Mungu. Na Musa alibarikiwa kumwona Mwenyezi Mungu, kumbukumbu zinasema, "uso kwa uso". Musa pia alikuwa rafiki yake Mwenyezi Mungu. (Taurati) Kutoka 33:11 "Naye BWANA [Mwenyezi Mungu] akasema na Musa uso kwa uso, kama vile mtu asemavyo na rafiki yake [Khalil]"...

Mtu mwingine aliyekuwa Khalil wa Mwenyezi Mungu ni Danieli, Nabii. Mara tatu [Taurati] inasema kwamba Mbingu zilimwona kuwa yeye ni 'mtu apendwaye sana'! (Taurati) Danieli 10:11 'Akaniambia, Ee Danieli, mtu upendwaye sana, yafahamu maneno nikuambiayo…' Angalia pia Danieli 9:23, na 10:19.

Kisha tunaye mtu aliyeitwa "Henoko". (Taurati) Mwanzo 5:24 'Henoko akaenda pamoja na [Mwenyezi] Mungu, naye akatoweka, maana [Mwenyezi] Mungu alimtwaa.' Kwa karibu mno Henoko alitembea na Mwenyezi Mungu hata hatimaye akamtwaa na kwenda naye kwake.

### *Mtu anakuwaje 'Rafiki' (Khalil) ya Mwenyezi Mungu?*

Je, hiyo ni kazi ngumu isiyowezekana? Hasha, vinginevyo hakuna ye yote miongoni mwa familia ya kibinadamu ambaye angepewa cheo kama hicho. Kwa hiyo, yatupasa kujitahidi kuwa miongoni mwa marafiki (Khalil) zake Mwenyezi Mungu kwa kuyachunguza maisha ya wale waliotangulia kupata cheo cha 'Khalil' au 'mtu apendwaye sana'.

Ibrahimu alimtii Mwenyezi Mungu katika maisha yake ya kila siku. Lo lote alilosema Mwenyezi Mungu, Ibrahimu hakuliamini tu na kulitii, bali alilitekeleza katika maisha yake. (Taurati) Mwanzo sura ya 12. Ibrahimu alipoitwa

kuiacha nchi yake, kufunga mizigo na kwenda, aliisikiliza sauti ya Mwenyezi Mungu na Ibrahimu akatii na kuiacha nchi yake. Akatekeleza matakwa ya Mwenyezi Mungu. Haidhuru yalikuwaje, Ibrahimu alimsikiliza kwa makini. Ibrahimu alitii kwa moyo wake wote, na kutekeleza kwa vitendo. Hivyo ndivyo ipasavyo kuwa kwa upande wetu tukitaka kuwa miongoni mwa 'Khalil', yaani, rafiki zake Mwenyezi Mungu wa karibu sana. Kama Mwenyezi Mungu amesema, basi, sharti tuwe tayari siyo kusikiliza tu, bali kutekeleza kwa vitendo yale aliyosema na kutekeleza matakwa yake.

Kuna walau mambo mawili ambayo ni lazima yatokee ili mtu apate kuwa 'Khalil' au rafiki wa karibu sana wa Mwenyezi Mungu.

Kwanza, lazima utii kamili uwepo na utii ambao hauna swali katika kufanya mapenzi ya Mwenyezi Mungu. Mwenyezi Mungu hatamlazimisha mtu ye yote kufanya kinyume cha nia yake.

Sura 002:256 'Hakuna kulazimishwa (mtu kuingia) katika dini.'… Sura 002:256 Al Baqarah

Hivyo utii huo kwa Mwenyezi Mungu hauna budi kuwa wa hiari utokao moyoni mwa mtu huyo, bila nguvu yo yote kutoka nje kutumika. Utii huu usio na masharti hautolewi tu kwa Mwenyezi Mungu, bali kwa huyo Neno aliyeteremshwa chini, pamoja na: (Taurati na Injili ya Maandiko ya Biblia), Taurati (Amri Kumi), Manabii, na Masihi Isa [Kristo Masihi] (huyo Neno atokaye kwa Mwenyezi Mungu)!

Sura 3:3 'Amekuteremshia Kitabu kwa haki, kinachosadikisha yaliyokuwa kabla yake. Na aliteremsha Taurati na Injili zamani - ziwe uongozi kwa watu. Na akateremsha vitabu vingine vya kupambanua baina ya haki na batili.' Sura 003:003 Aali Imran

Twaona katika Taurati mfano

mwingine wa mtu aliyemtii Neno aliyetoka kwa Mwenyezi Mungu. Jina lake alikuwa Hajiri, yule kijakazi, mke wa pili wa Ibrahimu. Hali ya maisha yake ilipokuwa haivumiliki katika maisha ya nyumbani mwa Ibrahimu, alikimbia kutokana na kunyanyaswa alikofanyiwa na Sarai, mke wa kwanza wa Ibrahimu. Alikimbilia jangwani, na ilikuwa dhahiri kwamba alikuwa akirudi kwao kule Misri. Malaika wa BWANA akakutana naye kule na kumwuliza… (Taurati) Mwanzo 16:8 'Akamwambia, Hajiri, wewe mjakazi wa Sarai, unatoka wapi, nawe unakwenda wapi? Akanena, Nakimbia mimi kutoka mbele ya bibi yangu Sarai.' Ndipo Malaika wa BWANA [Mwenyezi Mungu] alipomwambia arudi kambini kwa Ibrahimu na Sarai, na kunyenyekea chini ya mikono yake. Mwanzo 16:9 'Malaika wa BWANA [Mwenyezi Mungu] akamwambia, Rudi kwa bibi yako, ukanyenyekee chini ya mikono yake.' Kwa uaminifu akaitii sauti ya yule Malaika wa BWANA [Mwenyezi Mungu], akarudi na kunyenyekea. Huo ndio mwelekeo unaotupasa kuwa nao. Sharti tuwe tayari kuisikiliza sauti ya Mwenyezi Mungu na kunyenyekea kwa uaminifu kwake katika mambo yote. Swali moja linabaki, je, tutakuwa wakweli? Kutatokea nini endapo amri itokayo kwa Mwenyezi Mungu inakuja kwa njia tusiyotarajia? Je, hivi mimi bado nitabaki kuwa miongoni mwa 'Mutaqeen'? Hao ni wenye haki au wacha-Mungu (Mutaqeen) wanaofuata kwa uaminifu anakowaongoza Mwenyezi Mungu. Kumbuka kwamba Mwenyezi Mungu mawazoni mwake anakutakia wewe mambo mema kabisa. Ni kwa ajili ya usalama wetu milele.

Pili, yatupasa kujua mapenzi ya Mwenyezi Mungu ni nini! Twende wapi kutafuta maana ya mapenzi ya Mwenyezi Mungu? Kurani Tukufu yasema: 'Sema: "Tumemwamini Mwenyezi Mungu, na yale tuliyoteremshiwa na aliyoteremshiwa Ibrahimu na Ismaili na Ishaka na Yakubu na watoto (wake), na yale aliyopewa Musa na Isa na manabii (wengine) kutoka kwa Mola wao. Hatubagui baina yao hata mmoja, na sisi tunanyenyekea Kwake."' Sura: 003:-84 Aali Imran

Tunayaona mapenzi ya Mwenyezi Mungu yakiwa yamefunuliwa wazi kabisa katika Injili iliyoteremshwa kwetu kutoka kwa Masihi Isa (Kristo Masihi). 1 Wathesalonike 4:3 "Maana haya ndiyo mapenzi ya [Mwenyezi] Mungu, kutakaswa kwenu, mwepukane na uasherati." Utakaso ni utakatifu kwa Mwenyezi Mungu, utakatifu wa moyo na maisha! Ni kumruhusu Mwenyezi Mungu kuiandika Sheria yake ya Amri Kumi ndani ya mioyo yetu. Angalia jinsi maagizo yanayoeleweka wazi yalivyotolewa kwetu ili tuyafuate: (Taurati) Mhubiri 12:13 "Hii ndiyo jumla ya maneno; yote yamekwisha sikiwa; Mche [Mwenyezi] Mungu, nawe uzishike amri zake, maana kwa jumla ndiyo impasayo mtu." Isa, aliyeteremshwa kutoka kwa Mwenyezi Mungu alisema: Yohana 15:14 "Ninyi mmekuwa rafiki zangu, mkitenda niwaamuruyo." Kwa hiyo tunaona tunalo jukumu na ni wajibu wetu kumtii Mwenyezi Mungu kikamilifu, kushika Amri zake, na kuyatii Maneno yaliyoteremshwa kupitia Masihi Isa, hivyo ndivyo tunavyokuwa rafiki zake Mwenyezi Mungu kama alivyofanya Ibrahimu. Mwenyezi Mungu na akupe wewe Amani yake ya Milele!

## "Je! hivi wanaweza kusikia wale waliozikwa kaburini"?

Hili ni somo ambalo wengi wana utata nalo. Hata miongoni mwa waumini, jambo hili halieleweki wazi kwa wengi sana. 'Wafu wako wapi wanapoingia kaburini' na 'je! naweza kuongea nao'? Wengi wanazo hisia kwamba mtu afapo anaendelea kuishi katika hali fulani ya ulimwengu wa 'roho'. Kwamba bado yeye anaweza kuendelea kuongea na wapendwa wake. Somo hili ni la maana sana. Ni jambo la maana sana kwamba sisi tuijue kweli hii. Ibilisi (Shetani) anajua fika ya kwamba kama sisi tumechanganyikiwa na hatuna hakika juu ya jambo hili, basi yeye anaweza kutupotosha na tena atatupotosha. **Mara kwa mara Ibilisi atakuja hata kwa waumini na kuwafanya wafikiri kwamba bado wanaweza kuongea na wale waliokufa na kuingia makaburini mwao!** Ataweza hata kuja katika umbile la wapendwa waliokufa na kusema maneno fulani yahusuyo maisha yetu binafsi. Hivyo wengi wanashawishiwa kuamini kwamba kwa vile mengi yanajulikana kwa hao wanaodhaniwa kuwa ni wale waliokufa, basi ni lazima mambo hayo yawe ya kweli. Kwa njia hii mamilioni wanadanganywa na kufikiri kwamba wafu hawajafa kabisa, bali wamo katika hali nyingine ya maisha. Haya yote ni kama Shetani (Ibilisi) anavyotaka yawe. Kwa njia hiyo anaweza kuwadanganya watu wengi sana wa dunia hii kwa kuwaambia uongo, yaani, uongo ambao kama utasikilizwa na kuzingatiwa utawaongoza watu kwenda kwenye maangamizi yao ya milele.

### *Uongo wa Kwanza…*

Uongo wa kwanza uliowahi kusemwa duniani humu ulikuwa katika ile bustani nzuri ya Edeni. Wakati Ibilisi, kupitia ndani ya yule nyoka, alipoongea na Hawa, mwanamke yule wa kwanza. Akamwambia uongo. Kabla ya hapo, Mwenyezi Mungu alikuwa amemweleza Hawa waziwazi na kwa mkazo kwamba yeye wala mumewe hawakupaswa kula matunda ya mti ule mmoja "uliokatazwa ambao ulikuwa katikati ya ile bustani". Hivyo ndivyo Mwenyezi Mungu alivyonena nao na kuwaonya kwamba endapo wangeihalifu amri hii basi wangekufa. "Walakini matunda ya mti wa ujuzi wa mema na mabaya usile, kwa maana siku utakapokula matunda ya mti huo utakufa hakika." Taurati Mwanzo 2:17.

Ibilisi, akimtumia yule nyoka kama chombo chake, alisema na kukana yale Mwenyezi Mungu aliyokuwa ameyaeleza wazi, "Nyoka akamwambia mwanamke, Hakika hamtakufa" Taurati Mwanzo 3:4

### *Majibu yapatikane wapi?*

Tangu wakati ule wengi mno wameuamini uongo huo wa Ibilisi. Ibilisi ni baba wa uongo, kwa hiyo tusitazamie kitu cho chote kwake zaidi ya huo uongo. Leo tunataka kufanya utafiti wa vile **Vitabu Vitakatifu Taurati na Injili** ili kupata majibu kwa jambo hili la maana sana ambalo linaleteleza matokeo yatakayotuathiri milele. Ukweli wa Mwenyezi Mungu ni upi kuhusiana na wafu, na je! bado tunaweza kuendelea kuongea nao? Ili kupata hekima tumtafute Mwenyezi Mungu na njia yake. Yeye daima atawajulisha wale wanaonyenyekea chini ya mapenzi yake. Atawafunulia kweli yake wale wanaotaka

kwa dhati kujua yaliyo sahihi na ya kweli. Kumbukeni kile Nabii Muhammad alichokifunua katika Kurani Tukufu kwamba **Taurati** iliyoteremshwa kwa Musa na **Injili** iliyoteremshwa kwa Masihi Isa (Kristo Masihi) vilikuwa kwa mauidha yetu. Hivyo yeye alisema vilikuwa kwa uongozi, nuru, na kupambanua baina ya yaliyo ya haki na yasiyokuwa ya haki. Angalia: Sura 2:53 Al Baqarah, Sura 3:3 Aali Imran, Sura 21:48 Al-Anbiyaa

### *Ayubu mtumishi wa Mwenyezi Mungu!*

Katika Sura 38:41 twaambiwa tu"mkumbuke mja wetu Ayubu"… Kwa nini Ayubu ni wa maana? Alikuwa mmojawapo wa watu wale wa Kale wa Mashariki aliyetembea na Mwenyezi Mungu. Alipita katika majaribu ya kusikitisha, lakini alidumu kumshikilia Mwenyezi Mungu hata alipojaribiwa vibaya sana na Ibilisi (Shetani). Ayubu mtumishi wa Mwenyezi Mungu alikuwa nayo mengi ya kusema kuhusu wafu. Anatupa sisi mauidha yanayofaa sana siku hizi ambayo tunayahitaji ili kuzikwepa hila zake Ibilisi. Kwa maana Ibilisi anatafuta kuwadanganya wengi, hata ulimwengu mzima. Je, hivi tutayazingatia mauidha matakatifu aliyotupa mtumishi huyu mkuu wa Mwenyezi Mungu wa nyakati zile za Kale? Basi ni juu yetu kuyatii mauidha hayo na kwa unyenyekevu kuwa miongoni mwa wanaojifunza.

Je, wafu wanaweza kuongea na walio hai? Taurati Ayubu 14:7-14 'Kwani yako matumaini ya mti, ya kuwa ukikatwa utachipuka tena, wala machipukizi yake hayatakoma. Ijapokuwa mizizi yake huchakaa mchangani, na shina lake kufa katika udongo; Lakini kwa harufu ya maji utachipuka, na kutoa matawi kama mche. **Lakini mwanadamu hufa, huifariki dunia**; Naam, mwanadamu hutoa roho, naye *yupo* wapi? Kama vile maji kupwa katika bahari, na mto kupunguka na kukatika; ni

vivyo **mwanadamu hulala chini asiinuke; hata wakati wa mbingu kutokuwako tena**, **hawataamka, wala kuamshwa usingizini**. Laiti ungenificha kuzimuni, ukanilinda kwa siri, hata ghadhabu zako zitakapopita, na kuniandikia muda ulioamriwa, na kunikumbuka! Mtu akifa, je! atakuwa hai *tena*? Mimi ningengoja siku zote za vita vyangu, hata kufunguliwa kwangu kunifikilie."

Baada ya mtu kufa hataamka, mpaka wakati wa ufufuo. Analala kaburini na Mwenyezi Mungu ataweka wakati ambapo badiliko hilo litatokea. Badiliko hilo linahusu ufufuo, wakati ule Masihi Isa arudipo kuwaita waaminifu wa Mwenyezi Mungu ili wawe hai tena na kuwachukua kwenda nao paradiso ya mbinguni [peponi].

### *Ibilisi asichotaka wewe ujue!*

Ibilisi anataka watu waamini kwamba wanapokufa hawafi kabisa, bali wanaendelea kuishi mahali fulani. Huo ni udanganyifu ambao kwa huo mamilioni wanadanganywa. Lakini ukweli ni kwamba…

'**Mtu afapo, analazwa mahali pa kupumzikia kaburini, wala hana kabisa sehemu yo yote ya kufanya katika jambo lo lote litendekalo hapa duniani**'. Zingatia maneno haya ya Taurati: Mhubiri 9:5-6 "Kwa sababu walio hai wanajua ya kwamba watakufa; **lakini wafu hawajui neno lo lote**, wala hawana ijara tena; maana kumbukumbu lao limesahauliwa. Mapenzi yao na machukio yao, na husuda yao, imepotea yote pamoja; wala hawana sehemu tena katika jambo lo lote lililofanyika chini ya jua."

Ibilisi anazichukia aya hizi zitokazo katika Taurati kwa kuwa hawezi kuwadanganya wale wanaoielewa kweli hiyo. Ibilisi atakuja katika umbile lile lile la wapendwa wetu wale waliokufa, akiwa na kisa kilicho tofauti sana na kile tunachoendelea kujifunza hapa. Ni wakati ule tu tunapolindwa na kuongozwa na Vitabu hivyo Vitakatifu na kwa njia ya Roho [Ruh] wa Mwenyezi Mungu twaweza kusimama na kuyapinga madanganyo ya Ibilisi katika siku hizi za mwisho.

Yeye (Ibilisi) atatuambia kwamba wafu wanaweza kuongea na mwanadamu, na uongo mwingi unasemwa kwa watu na mara nyingi mno uongo huo unapokewa kama ndiyo kweli yenyewe.

035.022 "Wala hawawi sawa walio hai na wafu. Kwa yakini Mwenyezi Mungu Humsikilizisha Amtakaye; na wewe huwezi kuwasikilizisha waliomo makaburini. (Na hao kama wamekufa, wamo makaburini). Fatir 35:22

Je, Nabii Muhammad hakusema wazi juu ya jambo hili. Wale waliozikwa makaburini mwao hawawezi kusikia! Maisha yao yamekoma mpaka siku ya ufufuo. Hawana la ziada la kufanya tena katika jambo lo lote linalofanyika chini ya jua.

Masihi Isa alifundisha jambo lilo hilo, kwamba mtu anapokufa anaendelea kulala usingizi wa mauti mpaka hapo atakapoamshwa katika ufufuo. "Msistaajabie maneno hayo; kwa maana saa yaja, ambayo watu wote waliomo makaburini wataisikia sauti yake" [Mwenyezi Mungu]. Injili Yohana 5:28. Hivi wako wapi anapowaita Masihi Isa? Inaeleza waziwazi kuwa wamo makaburini mwao. Mpendwa, rafiki yake Mwenyezi Mungu, unapozikubali kweli za Neno la Mwenyezi Mungu utaelewa na kuwa na amani kuhusu wale wanaoingia makaburini. Sasa wao wanangoja Uumbaji Mara ya Pili au kufufuliwa kwa wafu ambako kunatokea anaporudi Masihi Isa.

053.047 "Na kwamba ni juu Yake ufufuo mwingine" (Uumbaji wa Pili); An-Najm

Je, Uumbaji huo wa Pili unatokea lini? Katika Injili twaambiwa kwamba… "Kwa dakika moja, kufumba na kufumbua, **wakati wa parapanda ya mwisho**; maana parapanda Italia, wa wafu watafufuliwa, wasiwe na uharibifu, nasi tutabadilika." Injili 1 Wakorintho 15:52. Unatokea parapanda ya Mwenyezi Mungu inapolia. Huna haja ya kuwa na wasiwasi kuwa utaikosa kwa maana utaisikia kwa hakika parapanda ile. Mwenyezi Mungu atahakikisha kwamba hakuna atakayekosa kuisikia katika tukio hili la ulimwengu mzima. Kwa huzuni leo wengi huenda mahali pale ambapo wafu wanadhaniwa kuwa wanapandishwa juu kwa ajili ya kutoa mauidha yao. Zamani watu wa Mwenyezi Mungu walikatazwa kwenda kuangalia mambo kama hayo. "Msiwaendee wenye pepo, wala wachawi; msiwatafute; ili kutiwa unajisi na wao; Mimi ndimi BWANA, Mungu wenu." Taurati Mambo ya Walawi 19:31. Kitendo kama hiki ni kufanya mawasiliano na Mapepo (Majini) yanayojigeuza na kufanana kabisa na wale waliokufa. Mwenyezi Mungu amekataza sana kufanya jaribio lo lote kama hilo la kuongea na waliokufa. Yule adui aliyeanguka, Ibilisi, husimama akiwa tayari kuwadanganya wote ambao hawatajali maagizo yaliyotolewa kwa makini ambayo yaliteremshwa kutoka kwa Mwenyezi Mungu. Leo hii Mwenyezi Mungu na akupe Amani yake ya Milele.

## Kitabu cha Mwenyezi Mungu

### *Je, Biblia ni Neno lake Mwenyezi Mungu?*

Je, Biblia yaweza kutegemewa? Je, hilo ni Neno litokalo kwake Mwenyezi Mungu? Haya ndiyo maswali ambayo mara kwa mara tunaulizwa na watu wengi siku hizi, hata na Waislamu wanauliza swali hili muhimu.

Hivi twawezaje kufahamu? Je, Maandiko ya Biblia yameteremshwa kweli kutoka kwa Mwenyezi Mungu? Sikuzote Mwenyezi Mungu hujibu maswali yaliyoulizwa kwa moyo mnyofu iwapo ombi linatoka katika kilio cha kweli cha kuijua ile kweli.

'Je, Nabii Muhammad alivionaje Vitabu Vitakatifu vya Maandiko ya Biblia'? Alilijibuje swali hili kuhusu "Taurati" na "Injili" [Maandiko ya Biblia]? Tunamwomba msomaji kuigeukia Kurani Tukufu na kuzipata aya zifuatazo:

### *Sura 2:53*

"Na (kumbukeni) Tulipompa Musa Kitabu (kilichokusanya kila wanayoyahitajia) na cha kupambanua baina ya yaliyo ya haki na yasiyokuwa ya haki ili mpate kuongoka." 2:053 Al-Baqarah. Sura 3:3 "Amekuteremshia Kitabu kwa haki, kinachosadikisha yaliyokuwa kabla yake. Na aliteremsha Taurati [ya Musa] na Injili [ya Yesu] zamani - ziwe uongozi kwa watu. Na akateremsha vitabu vingine vya kupambanua baina ya haki na batili. 003:003[-004] Aali Imran

Kurani Tukufu inataja kanuni moja tu ya kupambanua katika Hukumu, na hiyo ni Maandiko Matakatifu, Taurati. Katika Taurati tunauona msingi wa Hukumu, uitwao Amri Kumi. Huu ndio msingi wa serikali ya Mbinguni. Unapatikana katika (Taurati) Kutoka sura ya 20:1-17.

Sura 021:048 'Na kwa yakini tuliwapa Musa na Haruni (kitabu kilicho) kipambanuzi na mwanga na mauidha kwa wacha – Mungu.' 21:048 Al-Anbiyaa

Kurani Tukufu yatuambia kwamba Taurati ni Mwanga na Mauidha (Ujumbe) kwa wacha–Mungu. Anathubutuje, basi, mtu ye yote kuyadharau mauidha haya? Je, lisingekuwa jambo la kutisha kutoa mawazo yasemayo kwamba Taurati si Neno lake Mwenyezi Mungu? Sura 10:094 "Na kama unayo shaka juu ya hayo tuliyokuteremshia, basi waulize wale wasomao vitabu [Maandiko ya Biblia] kabla yako (Myahudi na Manasara wale waliosilimu). Kwa yakini haki imekwisha kukujia kutoka kwa Mola wako, kwa hiyo usiwe miongoni mwa wanaofanya shaka." Sura 010:094 Yunus

Hapa Nabii Muhammad amewaambia wasomaji "kuwauliza" wale ambao wamekuwa wakisoma Kitabu (Maandiko ya Biblia) kabla yao. Mbona Nabii huyu anayaelekeza mawazo yetu kwa wale wanaoiheshimu Biblia, isipokuwa kama alijua tu kuwa walikuwa sahihi?

### *Sura 005:044*

'Hakika tuliteremsha Taurati yenye uongozi na nuru; ambayo kwayo Manabii waliojisalimisha (kwa Mwenyezi Mungu) waliwahukumu Mayahudi: na watawa na maulamaa pia (walihukumu kwa hiyo Taurati), kwa sababu walitakiwa kuhifadhi Kitabu (hicho) cha Mwenyezi Mungu; nao walikuwa mashahidi juu yake. Basi (ninyi Waislamu) msiwaogope watu, bali niogopeni (mimi). Wala msibadilishe Aya zangu kwa thamani chache (ya duniani). Na wasiohukumu kwa yale aliyoteremsha Mwenyezi Mungu, basi hao ndio makafiri.' Sura 005:044 Al Maidah. Hizi ni baadhi tu ya sura nyingi zilizoorodheshwa katika Kurani Tukufu zishuhudiazo

kuwa Taurati na Injili viliteremshwa kutoka kwa Mwenyezi Mungu na ni kwa ajili ya watu wote (Binadamu). Hapa inaiita Taurati kuwa ni "Kitabu cha Mwenyezi Mungu".

Baadhi ya watu wangependa kutoa hoja zao kwamba Biblia imebadilishwa na kuchafuliwa, yaani, kwamba haiwezi kutegemewa tena? Kwa usemi huo, twauliza swali rahisi. Kama Biblia ilikuwa imebadilishwa kabla ya kipindi cha Muhammad kwa kiwango ambacho isingeweza kutegemewa tena, basi, kwa nini Nabii huyu aliyaelekeza sana mawazo ya watu kwenye [kitabu] hicho? Je, Mwenyezi Mungu angemwelekeza Nabii huyu kwenye kitabu hiki cha uongo kilichochafuliwa? Hasha! hili huonesha tu kwamba Maandiko ya Biblia yaliaminika katika kipindi kile cha Muhammad.

Hivyo, basi, endapo Maandiko ya Biblia yangekuwa yamechafuliwa tangu kipindi kile cha yule Nabii Mstahiki, basi yako wapi maandiko ya mkono ambayo ni ya kweli? Hakuna hata mmoja aliyeweza kuonesha maandiko ya mkono kama hayo kwa sababu hayako. Maandiko ya Biblia yale yale yaliyokuwako wakati wa Muhammad ndiyo yale yale ambayo bado yanapatikana leo. Kumbuka kwamba Mwenyezi Mungu anaweza kuyahifadhi Maneno yake yasichafuliwe ili mwanadamu leo apate kuyajua Mapenzi ya Mwenyezi Mungu. Zaidi ya haya yote, nani angeweza kufanya kazi ngumu ya kuyatafuta maandiko yote ya mkono ya Biblia na kuyakusanya pamoja ili kuyabadilisha au kuyafanya ya uongo? Fikiria kwa makini sana juu ya jambo hili mpendwa msomaji!

Mauidha yaliyo katika Injili bado yanadumu kuwa ya kweli leo. (Injili) Mathayo 4:4 'Yesu [Masihi Isa] akamjibu, Imeandikwa ya kwamba mtu hataishi kwa mkate tu, ila kwa kila neno la [Mwenyezi] Mungu.'

Kwa salama sisi twaweza kuliamini Neno lake. Ninao ushuhuda wangu binafsi kuhusu kile Neno la Mwenyezi Mungu, yaani, Biblia, lilichonifanyia mimi. Kujifunza Kitabu hiki hubadilisha maisha. Katika kurasa za Kitabu hiki (Maandiko ya Biblia) umo uwezo, yaani, nguvu inayotolewa kwa wale wanaotumia muda wao kufahamu yaliyomo. Mabadiliko yanaonekana dhahiri. Kwake yeye anayetii Maneno haya ya Mwenyezi Mungu atagundua kwamba mtu anapata mwonjo mpya, mawazo mapya, hisia mpya, makusudi mapya yatakayoyaongoza maisha yake. Haya yote hutokea unapomtii Mwenyezi Mungu na Neno Lake aliloliteremsha.

(Injili) Yohana 6:63 'Roho ndiyo itiayo uzima, mwili haufai kitu; maneno hayo niliyowaambia ni roho, tena ni uzima'. Masihi Isa alisema waziwazi ya kwamba maneno hayo ni 'roho' na tena ni 'uzima'.

Wenye hekima kutoka Mashariki wa zamani waliiona thamani ya Neno la Mwenyezi Mungu. (Taurati) Ayubu 22:22 "Uyapokee, tafadhali, mafunzo (Taurati) yatokayo kinywani mwake, na maneno yake yaweke moyoni mwako.'

Tena Ayubu anatuambia kwamba … "Sikurudi nyuma kuiacha amri ya midomo yake; Nimeyatunza maneno ya kinywa chake zaidi ya riziki yangu." (Taurati) Ayubu 23:12.

Hatuhitaji kuwa na hofu kwamba Neno la Mwenyezi Mungu lingeweza kuchafuliwa. Je, Mwenyezi Mungu si anao uwezo usio na kikomo? Je, hawezi kutegemewa kuwa atalihifadhi Neno lake leo kwa ajili yetu hapa duniani?

Sura 6:115 'Na yametimia maneno ya Mola wako kwa kweli na uadilifu. Hakuna awezaye kuyabadilisha maneno Yake. Na Yeye ndiye asikiaye (na) ajuaye.' 6:115 Al An-am

Kwa bahati mbaya wengi wamelitangua Neno la Mwenyezi Mungu kwa mapokeo waliyopokea yasiyo na msingi wo wote katika vile Vitabu Vitakatifu. Tunahitaji kuwa waangalifu sana mauidha haya yasije yakatuhusu na sisi … (Injili) Marko 7:13 "Huku mkilitangua Neno la Mungu kwa mapokeo yenu mliyopokeana; tena mwafanya mambo mengi yaliyo sawasawa na hayo.' Maneno haya ya onyo yatokayo kwa Masihi Isa yanatuhusu sisi pia kama wale wa siku zile. Hebu na tulizingatie onyo hilo. Siku ile itakuwa ya kutisha jinsi gani tukijikuta tumeyatangua Maneno ya Mwenyezi Mungu!

Rafiki zangu, sasa kuliko wakati mwingine wo wote uliopita ni wakati wa kulizingatia kwa njia ya pekee lile Neno lililoteremshwa kwetu (Taurati na Injili). Kila siku maneno yake yazame ndani kabisa ya mioyo yetu. Mwenyezi Mungu na ayabadilishe maisha yenu ili ninyi pia mweze kutoa ushuhuda kwamba kweli haya ni Maneno yatokayo kwa Mwenyezi Mungu … na ya kwamba yanaweza kututayarisha kukabiliana na siku za usoni bila ya kuogopa.

(Injili) 2 Timotheo 3:16-17 "Kila andiko, lenye pumzi ya Mungu, lafaa kwa mafundisho, na kwa kuwaonya watu makosa yao, na kwa kuwaongoza, na kwa kuwaadibisha katika haki; ili mtu wa Mungu awe kamili, amekamilishwa apate kutenda kila tendo jema." (Taurati) Isaya 40:8 "Majani yakauka, ua lanyauka; Bali Neno la [Mwenyezi] Mungu wetu litasimama milele".

Neno La Mwenyezi Mungu kama lilivyoandikwa katika Taurati na Injili ndicho "Kipimo", kinachoonesha kama Mjumbe huyo anafundisha au hafundishi kweli. (Taurati) Isaya 8:20 "Na waende kwa Sheria na Ushuhuda; ikiwa hawasemi sawasawa na Neno hili, bila shaka kwa hao hapana asubuhi."

## "Msiruke Mipaka kwa (kuvunja taadhima ya) Jumamosi [Sabato]"

Je, Waislamu wanapaswa kuitunza siku ya Sabato "Sabt" kama siku ya kupumzika ambayo mtu hujizuia asifanye kazi yo yote?

Wengi katika dini ya Kiislamu huamini kwamba zile Amri Kumi zilizoandikwa kwa "kidole chake Mwenyezi Mungu" hazina budi kutiiwa. Kile ambacho wengi wamepitiwa ni ukweli kwamba moja wapo ya hizi "Amri Kumi" imesahauliwa. Hata Wakristo wengi wanaodai kukifuata Kitabu hicho (Vitabu Vitakatifu vya Biblia) hawaijali moja ya hizo Amri kama zilivyoandikwa katika Taurati. Kusema kweli wengi wao wanaziangalia kwa chuki kubwa au kwa dharau kubwa Sheria hizo ambazo ni Takatifu kwa wanadamu.

Kwanza, twataka kujadili hoja hii, Je, Amri Kumi ni nini? Je, hivi yatupasa kuishi kwa kuzifuata sheria hizi siku hizi? Twataka kuziangalia kwa makini hizo Amri Kumi kuona ni nini hasa. Zimeandikwa katika Taurati katika Kutoka 20 na Kumbukumbu la Torati 5 la (Vitabu Vitakatifu) na katika Injili yote ya Maandiko ya Biblia. Mkumbukeni Mstahiki Nabii Muhammad kile alichokifunua katika Kurani Tukufu kwamba Taurati iliyoteremshwa kwa Musa na Injili aliyopewa Masihi Isa, vyote viwili vilikuwa kwa ajili ya mauidha kwetu. Hivyo kwetu ni uongozi, nuru, na kipimo cha hukumu. Angalia:

Sura 2:53 Al Baqarah; Sura 3:3 Aali Imran; Sura 21:48 Al-Anbiyaa; Sura 10:94 Yunus; Sura 5:44 Al Maidah.

Sura hizi ni baadhi tu ya kumbukumbu nyingi zilizomo ndani ya Kurani

Tukufu kuhusu hivyoVitabu Vitakatifu vya Maandiko ya Biblia (Taurati na Injili).

Kielelezo cha Ibrahimu…

Watu wengi leo huona kwamba Ibrahimu yule wa zamani, alikuwa ni mtu aliyemheshimu Mwenyezi Mungu kwa moyo wake wote. Hivyo yeye amekuwa kielelezo fulani kwetu cha kufuata. Katika Vitabu vile Vitakatifu (Maandiko ya Biblia) twaambiwa yafuatayo kuhusu Ibrahimu na jinsi alivyoziona zile Amri Kumi za Mwenyezi Mungu. Taurati, Mwanzo 26:5 "… Ibrahimu alisikia sauti yangu, akayahifadhi maagizo yangu, na amri zangu, na hukumu zangu, na sheria zangu." Aya hii katika Taurati hutuambia kwamba Amri Kumi za Mwenyezi Mungu zilifuatwa na Ibrahimu aliyeishi muda mrefu kabla ya siku za Musa. Hiyo pia inatuambia sisi ya kwamba watu wa nyakati zile za kale waliijua fika sheria ile ile ambayo pia ilirudiwa kwa Musa katika vilele vile virefu vya Mlima Sinai. Iwapo Ibrahimu anafikiriwa kuwa ni "Hanif" kati ya wale ambao kwa unyofu wa moyo wanamkaribia sana Mwenyezi Mungu, basi, sisi tungefanya vema kukifuata kielelezo chake Ibrahimu kwa kuzitunza pia Amri Kumi za Mwenyezi Mungu. Kufanya mambo yawe rahisi, hii maana yake ni kwamba Ibrahimu aliitunza Siku ya Saba ya juma kama siku ya 'kupumzika' kwa heshima yake Mwenyezi Mungu

### *“Kidole chake Mwenyezi Mungu”*

Kisa cha Amri Kumi kimeandikwa katika Taurati (Kutoka 20). Wana wa Israeli waliokuwa wameokolewa kutoka utumwani Misri walipofika jangwani, Musa aliagizwa kwenda juu ya Mlima Sinai. Ni wakati ule alipokuwa kule alipopewa mbao mbili za mawe ambazo juu yake ziliandikwa zile Amri (Maneno) Kumi kwa kidole chake Mwenyezi Mungu. Kutoka 31:18 na Kumbukumbu la Torati 9:10. “Na tukaunyanyua mlima juu yao (hao Mayahudi) kwa kufanya agano nao (la kufuata Taurati). Na tuliwaambia: ‘Liingieni lango (la nchi ya Shamu) hali ya kuinama (kama mnarukuu)”; (wakapinga). Na (pia) tukawaambia: “Msiruke mipaka kwa (kuvunja taadhima ya) Jumamosi [Sabato].’ ‘Na tukachukua kwao ahadi iliyo madhubuti’ ...” Sura 004:154 (An-Nisaa [Wanawake]).

Je, Mwenyezi Mungu angemwita mtu Mnafiki kuwa ni Mtume wake?

Hili ni swali ambalo wengi wenu kwa hakika tayari mnalijua jibu lake. Hasha! Lakini basi, hatuna budi kujiuliza swali hili: Kama Nabii Mstahiki Muhammad angeweza kusema “Msiruke mipaka” katika suala la Sabato, je, si angeitwa kuwa ni ‘mnafiki’ endapo yeye mwenyewe asingeitunza hiyo Sabato? Kwa maneno mengine, Nabii huyu Mstahiki asingewataka watu kutii mojawapo ya Amri za Mwenyezi Mungu wakati yeye mwenyewe haitii sheria hiyo! Kwa ajili hii ushahidi upo wa kutosha kuwa huyo Nabii Mstahiki Muhammad ni lazima alikuwa ameitii pia ile Amri ya nne. Amri hii inatuambia kupumzika Siku ya Saba ya juma kwa heshima yake Mwenyezi Mungu na kutusaidia kukumbuka kwamba Mwenyezi Mungu aliumba vitu vyote kwa siku sita. Katika maneno yaliyo dhahiri kabisa kutoka katika Kurani Tukufu imeandikwa kwamba Sabato isivunjwe, kwa kweli katika sura ifuatayo “laana” ilitamkwa na Mwenyezi Mungu juu ya wale waliokuwa “wavunjaji wa Sabato’. “Enyi mliopewa Kitabu! Aminini tuliyoyateremsha yanayosadikisha yale yaliyo nanyi, kabla hatujazigeuza nyuso tukazipeleka kisogoni, au kabla ya kuwalaani kama tulivyowalaani watu (walioharibu utukufu) wa Jumamosi. Na amri ya Mwenyezi Mungu lazima kufanywa.” Sura 004:047 (An-Nisaa [Wanawake]).

### *Kielelezo cha Masihi Isa…*

Pengine kutoka kwa yule Mmoja aliyekuwa karibu sana na Mwenyezi Mungu twaweza kujifunza ukweli kuhusu Sabato na kama bado inafanya kazi yake hadi leo! Tunacho kielelezo chake Masihi Isa aliyeteremshwa kutoka kwa Mwenyezi Mungu ambaye alikuwa ndiye lile Neno kutoka kwa Mwenyezi Mungu. Ni kwa Masihi Isa Injili ilitolewa. Katika Sura 3:45 twaambiwa kwamba Neno kutoka kwa Mwenyezi Mungu lilikuja kwa njia ya Masihi Isa aliyepewa heshima. Kutoka kinywani mwa yule aliyeteremshwa chini tunayo kumbukumbu isemayo kwamba ... Siku ya Sabato Isa alifundisha katika sinagogi. (Injili) Marko 1:21 “Wakashika njia mpaka Kapernaumu, na mara siku ya Sabato [Masihi Isa] akaingia katika sinagogi, akafundisha.”

Lakini watu wengine wanataka kutoa hoja hii kwamba Sabato ilifanywa kwa ajili ya Wayahudi tu … lakini lile Neno kutoka kwa Mwenyezi Mungu lilisema haya yafuatayo: (Injili) Marko 2:27 “Akawaambia, Sabato ilifanyika kwa ajili ya mwanadamu, si mwanadamu kwa ajili ya Sabato.”

Wengine wangependa kupotosha au kunukuu vibaya fungu hili ili lisomeke ‘Myahudi’ badala ya kusomeka ‘mwanadamu’. Lakini hapo limeandikwa katika lugha inayoeleweka kwamba Masihi Isa aliyeteremshwa chini kutoka kwa Mwenyezi Mungu na ambaye alikuwa miongoni mwa wale waliokuwa karibu sana na Mwenyezi Mungu, na kupewa heshima… (Sura 3:45), ametuambia kweli ya kwamba ‘Sabato ilifanyika kwa ajili ya mwanadamu’. Mwanadamu huyo anamaanisha binadamu wote. Lakini ni waumini wangapi wanaoutii ujumbe huu utokao kwa Mwenyezi Mungu? Je, watu hawaoni kuwa shughuli zao binafsi ni za maana kuliko shughuli yake Mwenyezi Mungu, katika hiyo Siku Yake Takatifu, ya Saba katika juma (Jumamosi), iitwayo ‘Sabt’ (Sabato)? Wengi wanavifanya hivyo Vitabu Vitakatifu kuwa kama ‘ubao wa kubashiria’ ambao juu yake unachagua kile unachotaka. Unachagua baadhi ya vitu na kuvikataa vingine. Je, hayo siyo yaliyokwisha kutokea katika ulimwengu wetu wa leo? Yuko wapi mtafutaji wa ile kweli aliye makini? Ni akina nani miongoni mwa watu ambao huyapa kipaumbele mambo ya Mwenyezi Mungu, na kutafuta kwa moyo wao wote kuyajua mapenzi yake? Katika Injili, Mathayo 4:4 inasomeka hivi … “Mtu hataishi kwa mkate tu, ila kwa kila neno litokalo katika kinywa cha [Mwenyezi] Mungu.” Kwa hiyo sisi hatujaachiwa [kazi ya] kuchambua na kuchagua wenyewe.

Je, Mwenyezi Mungu ni Kigeugeu?

Taurati Kumbukumbu la Torati 5:22 “Haya ndiyo maneno ambayo BWANA [Mwenyezi Mungu] aliwaambia mkutano wenu wote mlimani kwa sauti kuu toka kati ya moto, na wingu, na giza kuu; wala hakuongeza neno. Akayaandika juu ya mbao mbili za mawe, akanipa [mimi Musa].” Kutoka 20:1 “[Mwenyezi] Mungu akanena maneno haya yote akasema” … Hivyo Mwenyezi Mungu hakunena tu yale Maneno, bali pia aliyaandika Maneno yale ili sisi tusikosee. Hapa chini limenukuliwa Neno lililotoka kwake Mwenyezi Mungu. (Taurati) Kutoka 20:8-11 ‘Ikumbuke siku ya Sabato uitakase. Siku sita fanya kazi, utende mambo yako yote; lakini siku ya saba ni Sabato ya BWANA, Mungu wako, siku hiyo usifanye kazi yo yote, wewe, wala mwana wako, wala binti yako, wala mtumwa wako, wala mjakazi wako, wala mnyama wako wa kufuga, wala mgeni aliye ndani ya malango yako. Maana, kwa siku sita BWANA alifanya mbingu, na nchi, na bahari, na vyote vilivyomo, akastarehe siku ya saba; kwa hiyo BWANA akaibarikia siku ya Sabato akaitakasa.’

Zingatia, Ee mpendwa msomaji , Mwenyezi Mungu aliibariki siku ile na kuitakasa.

Je, hivi Mwenyezi Mungu atazibadili au kuzigeuza Sheria zilizotoka mdomoni mwake? Zaburi 89:34 “Mimi sitalihalifu agano langu, Sitalibadili Neno lililotoka midomoni mwangu.” Pia [soma] hapa: 1 Mambo ya Nyakati 17:27 “Nawe sasa umekuwa radhi kuibarikia nyumba ya mtumwa wako, ipate kudumu milele mbele zako; kwa maana wewe, BWANA, umebarikia, nayo imebarikiwa milele.” Basi, ni juu yetu kuchagua iwapo tutafuata na kutii kwa ukamilifu mapenzi yake au je, sisi twafanana na wasioamini wanaoyadharau Mapenzi yake Mwenyezi Mungu? Hebu na tuonekane miongoni mwa walio waaminifu, hili ndilo ombi letu kwako mpendwa msomaji. Kumbuka kwamba Mwislamu ni mtu anayelitii Neno lake Mwenyezi Mungu bila swali, je, hilo lisingeihusu [pia] Sabato?

### ‘Mwenyezi Mungu … asafishe yaliyo mioyoni mwenu.’

Mbona siku hizi kuna udanganyifu mwingi mno, rushwa, na uhalifu katika jamii? Hata wale wanaoonekana kana kwamba ni wanadini wema hawajaachwa wasipatwe na matatizo haya. Je, maradhi haya yametoka wapi? Hivi Mwenyezi Mungu aliiumba mioyo ya binadamu kuwa na ufisadi kama huo? Au ni wanadamu wenyewe waliochagua mambo kuwa hivyo? Haya ni baadhi tu ya maswali tunayotafuta majibu yake.

‘Amekuteremshia Kitabu kwa haki, kinachosadikisha yaliyokuwa kabla yake. Na aliteremsha Taurati na Injili zamani - ziwe uongozi kwa watu. Na akateremsha vitabu vingine vya kupambanua baina ya haki na batili.’

Al-Quran, 3:3 (Aali Imran).

Kurani Tukufu yatuambia sisi kwamba Sheria (Taurati) na Injili ni uongozi kwa watu. Mwenyezi Mungu ametupa nuru na uongozi katika kile ambacho Kurani Tukufu inakiita “Kitabu chake Mwenyezi Mungu” [yaani, Taurati ya Maandiko Matakatifu] Sura 5:44, hayo alipewa Musa. Walakini, Mungu hakukomea pale, pia alitupa Injili kuwa uongozi, nuru, mauidha na kutuhakikishia yaliyoteremshwa kabla yake katika Taurati au Kitabu chake Mwenyezi Mungu. Kitabu cha Mwenyezi Mungu kinayo majibu tunayohitaji kwa maswali haya magumu. Kama Maneno yaliyoteremshwa kwetu

katika Taurati na Injili yangekuwa hayajatoka kwa Mwenyezi Mungu, basi, Nabii Mstahiki Muhammad asingekuwa ametupa mauidha mengi mno kutuelekeza kwenye hivi Vitabu Vitakatifu. Kwa hiyo tunamwona Nabii Mstahiki Muhammad akituelekeza tena na tena kwenye Vitabu hivi Vitakatifu vya Maandiko ya Biblia. [Sura 5:44-48, Sura 21:48].

## *Jinsi Moyo wa Binadamu Ulivyopata Ugonjwa…*

Wengi wenu mnakijua kisa cha Adamu, yule binadamu wa kwanza aliyeumbwa na Mwenyezi Mungu. Kisa chote kimeandikwa katika Taurati (Mwanzo 1:26-31). Mwenyezi Mungu alikuwa amemwumba Adamu na mkewe wakiwa wakamilifu na watakatifu. Akawaweka katika bustani nzuri. Walipaswa kufurahia raha na utulivu wa mbinguni. Hakuna cho chote kilichovuruga amani yao. Asili zao zilikuwa safi, mawazo yao yalikuwa matakatifu. Mwenyezi Mungu aliwapa vitu vyote walivyoweza kuhitaji katika bustani hii nzuri ili kuwafurahisha. Waliruhusiwa kula matunda ya miti yote waliyopewa kuwa chakula chao … isipokuwa ule mmoja. Kitu kimoja tu walizuiwa … yaani, walikatazwa wasile matunda ya 'mti wa ujuzi wa mema na mabaya' uliokuwa katikati ya bustani ile. Taurati (Mwanzo 2:15-17) 'Walakini matunda ya mti wa ujuzi wa mema na mabaya usile, kwa maana siku utakapokula matunda ya mti huo utakufa hakika.' Hili lilikuwa ni jaribio tu la imani kuona kama mtu yule ataweza kutegemewa.

Mambo yote yakawaendea vizuri, mume yule na mkewe, katika bustani ile ya raha (peponi), isipokuwa siku ile walipoasi. Sasa mawazo ya Adamu hayakuwa safi tena kwa asili yake kama yalivyokuwa hapo mwanzo, bali yakawa maovu. Tangu siku ile hadi siku hizi zetu dhambi imewaletea wanadamu wote laana. Kwa kuwa tu watoto tuliotoka kwa Adamu, sisi pia tumerithi asili yake iliyoanguka dhambini. Katika Taurati tunaambiwa juu ya hali yetu ilivyo hasa. Yeremia 17:9 'Moyo [wa mwanadamu] huwa mdanganyifu kuliko vitu vyote, una ugonjwa wa kufisha; nani awezaye kuujua?'

## *Uponyaji unavyokuja…*

Mioyo yetu (mawazo yetu) haiwezi kutegemewa, hatuwezi kuangalia ndani yetu wenyewe na kudhani twaweza kutatua matatizo yetu. Hakuna tiba ya kibinadamu iliyopatikana kutibu hali ya dhambi iliyo ndani ya moyo wa mwanadamu. Mwenyezi Mungu hakumwacha mwanadamu katika hali isiyo na matumaini. Ameahidi kutusaidia. Je, haya si maneno ya faraja,… "Mwenyezi Mungu ili ayadhihirishe yaliyomo vifuani mwenu, na asafishe yaliyo mioyoni mwenu. Na Mwenyezi Mungu anayajua (hata) yaliyomo vifuani." Al-Qur'an, 003:154 (Aali Imran). Ni Mwenyezi Mungu anayechukua hatua ya kwanza kumsaidia mwanadamu. Hata hivyo, mwanadamu sharti atake kusafishwa, yaani, apate utakaso utokao kwa Mwenyezi Mungu. Mwanadamu hana budi kuomba kwa ajili ya jambo hilo, na kulitafuta kwa uwezo wake wote. Lakini je, huko kutakaswa kwa moyo wa kibinadamu kunawezaje kufanyika na kwa njia ya nani? Kurani Tukufu inaongea juu ya Mmoja aliyeteremshwa hapa chini kutoka kwa Mwenyezi Mungu. Huyo Mmoja wa pekee aliyekuwa karibu sana na Mwenyezi Mungu, jina lake ni Masihi Isa. "(Kumbukeni) waliposema Malaika: "Ewe Maryamu! Mwenyezi Mungu anakupa habari njema (za kumzaa mtoto bila ya mume, bali kwa kutamkwa) Neno tu litokalo kwake (la kukwambia 'Zaa' ukazaa pasina kuingiliwa). Jina lake ni Masihi, Isa, mwana wa Maryamu, mwenye heshima katika dunia na Ahera, na miongoni mwa waliopelekwa mbele na Mwenyezi Mungu." Sura 3:45 (Aali Imran).

Twasoma kwamba Masihi Isa alikwenda huku na huku akiwa na huruma kwa watu, akiponya magonjwa yao. Je, yawezekana kwamba huyu Mmoja aliyeteremshwa kutoka kwa Mwenyezi Mungu angeweza pia kuponya ugonjwa huo wa moyo? Twasoma katika Injili, kwamba wote waliokuja kwake Masihi Isa kwa uponyaji wa matatizo ya kimwili na kiakili walipewa msaada. Hakuna hata mmoja aliyefukuzwa. Twasoma katika Vitabu Vitakatifu, (Injili) Marko 1:41 "Naye [Masihi Isa] akamhurumia [mwenye ukoma], akanyosha mkono wake, akamgusa, akamwambia, Nataka, takasika." Je, hivi kungekuwa na uwezekano pia kwamba Mwenyezi Mungu afanye ipatikane tiba ya ugonjwa uliomo ndani ya moyo wa mwanadamu kwa ajili yetu kupitia kwa mtu yuyo huyo Masihi Isa? Katika Injili tunaambiwa tena, 1 Yohana 1:7 'Bali tukienenda nuruni, kama yeye (Masihi Isa) alivyo katika nuru, twashirikiana sisi kwa sisi, na damu yake Yesu (Masihi Isa), Mwana wake, yatusafisha dhambi yote."

Hili ni jambo tunaloweza kulionja sasa hivi. Kusafishwa mazoea yote mabaya na matendo mabaya, hata na mawazo yetu machafu yanayotushikilia katika maovu. Mazoea yetu mabaya yawe ni mawazo maovu au matendo maovu, kusema uongo, kukosa uaminifu, uzinzi, yote haya, na mengine mengi, Mwenyezi Mungu anajua yaliyomo mioyoni mwetu. Mwenyezi Mungu analo suhulisho, tena ameahidi kutuweka huru mbali na maradhi hayo ya dhambi. Hii ndiyo maana Masihi Isa anaitwa "Masihi" "Mwokozi" atuokoaye sisi kutoka katika dhambi. Siyo tu kwamba Isa alilipa fidia kwa ajili ya dhambi zetu, bali pia mtu huyu aliyeteremshwa kutoka kwa Mwenyezi Mungu alituahidi kutupa moyo mpya, kuponya ugonjwa katika mioyo yetu iliyoanguka dhambini. Twapokea msaada tu tukienda kwa Mwenyezi Mungu na kwake Yeye ambaye Mwenyezi Mungu alimteremsha. Injili 1 Tim. 2:5-6: "Kwa sababu Mungu ni Mmoja, na mpatanishi (Shafi) kati ya Mungu na wanadamu ni mmoja, Mwanadamu Kristo Yesu (Masihi Isa); ambaye alijitoa mwenyewe kuwa ukombozi kwa ajili ya wote"..,

## *Usafishaji huo wa moyo ni mkamilifu jinsi gani?*

Kwa kiwango kile cha kuyageuza hata mawazo yetu yenyewe! 2 Wakorintho 10:5 [Injili] 'Tukiangusha mawazo na kila kitu kilichoinuka, kijiinuacho juu ya elimu ya [Mwenyezi] Mungu; na tukiteka nyara kila fikira ipate kumtii Kristo [Masihi Isa]…' Injili Matendo 3:26 "[Mwenyezi] Mungu, akiisha kumfufua mtumishi wake Yesu [Masihi Isa], alimtuma kwenu ninyi kwanza [Waisraeli], ili kuwabarikia kwa kumwepusha kila mmoja wenu na maovu [dhambi] yake."

Katika siku za nyuma watu hawakumtaka Mwokozi kama huyo, walichagua kubaki katika dhambi na kubaki na ugonjwa wa moyo ulio na dhambi. Kwa kweli wale walioutangaza ujumbe huu wa uhuru walichukiwa sana sana na Wayahudi, kiasi kwamba wengi walifungwa gerezani na hata kuuawa. Hiyo ilikuwa ndiyo chuki dhidi ya wale waliompokea Yeye ambaye Mwenyezi Mungu alimteremsha kuja katika dunia hii. Kwa kweli wafuasi wa Masihi Isa walinena kwa ujasiri mno kiasi cha kutangaza kwamba… "wala hakuna wokovu katika mwingine awaye yote, kwa maana hapana jina jingine chini ya mbingu walilopewa wanadamu litupasalo sisi kuokolewa kwalo." Matendo 4:12 Injili. Basi, kwa heshima yake, je, waona ni ajabu kwamba Muhammad aliitaja Injili … yaani, kwamba hii ilikuwa ndiyo 'injili' au habari njema iliyoteremshwa chini kutoka kwa Mwenyezi Mungu kupitia Masihi Isa? Kwa nini Nabii Muhammad amtaje Masihi Isa katika Sura zipatazo kumi na tano pamoja na kumtaja Isa zaidi ya mara 90 katika Kurani Tukufu? Hakika habari zilizo katika Injili ni "Habari Njema kutoka kwa Mwenyezi Mungu". Sura 3:45

## *Moyo wako uwezavyo kupokea mbaraka huo…*

Moyo wa zamani wenye dhambi hauna tiba ya kibinadamu… Tujaribu sana kama tuwezavyo kutenda matendo mema, na kuwapa maskini msaada, na kuomba mara kwa mara na kwa muda mrefu … hata hivyo mambo hayo hayawezi kutakasa maisha yetu. Hatuwezi kuugeuza moyo wetu

wa kibinadamu kwa kutenda matendo mema na kuomba sala ndefu … Mwenyezi Mungu peke yake ameahidi kuuponya moyo huo mgonjwa kwa kutupa moyo mpya … (Taurati) Ezekieli 36:26 'Nami nitawapa ninyi moyo mpya, nami nitatia roho mpya ndani yenu, nami [Mwenyezi Mungu] nitatoa moyo wa jiwe [mgumu na uliojaa ufisadi] uliomo ndani ya mwili wenu, nami nitawapa moyo wa nyama.'

Hivi twawezaje kuwa na huo 'moyo mpya'? Kwa kumwomba tu Mwenyezi Mungu! Nenda kwake faraghani na kufanya maombi (dua) au wakati unapokuwa Msikitini. Mwenyezi Mungu ni mwingi wa rehema, mpole, na mwenye huruma kwa watoto wote wa wanadamu. Lakini hatumii nguvu kuja kwetu. Katika Kurani Tukufu amesema … 'Hakuna kulazimishwa (mtu kuingia) katika dini. Uongofu umekwisha pambanuka na upotofu. Basi anayemkataa shetani na akamwamini Mwenyezi Mungu, bila shaka yeye ameshika kishiko chenye nguvu kisichokuwa na kuvunjika. Na Mwenyezi Mungu ni mwenye kusikia mwenye kujua.' Sura 2:256 (Al Baqarah).

Vivyo hivyo Mungu hatatumia nguvu juu yetu, anapaswa kuombwa. Mjumbe wake wa kibinadamu peke yake sharti afanye uamuzi na kumwomba. Mwanadamu sharti achague nani atakayekuwa Bwana wake. Ama ni Mwenyezi Mungu kupitia Masihi Isa, ama, ni Shetani (Ibilisi) yule aliyeanguka, ambaye ni laghai mkuu. Mamlaka zote za Mbinguni zinahusika katika kukusaidia wewe kufanya uamuzi huo. Mwombe leo hii! Shika 'kishiko kile chenye nguvu kisichokuwa na kuvunjika'.

## 'Tukamkomboa kwa Mnyama wa Kuchinjwa Mtukufu'!

Kurani Tukufu inatoa mfano halisi ulio kielelezo cha utii wetu kwa Neno atokaye kwa Mwenyezi Mungu wakati Ibrahimu alipoitwa kuiacha nchi yake, jamaa zake, nyumba yake, naye akatakiwa kwenda mahali ambako Mwenyezi Mungu angemwambia. Ibrahimu alitii bila swali Mwenyezi Mungu aliponena naye. Hayo yameandikwa katika Mwanzo 12:1 (Taurati) "BWANA akamwambia Abramu [baadaye aliitwa Ibrahimu], Toka wewe katika nchi yako, na jamaa zako, na nyumba ya baba yako, uende mpaka nchi nitakayokuonesha." Taurati inaendelea kuandika habari za Ibrahimu alivyoitikia … Mwanzo 12:4 "Basi Abramu akaenda, kama BWANA alivyomwamuru … Naye Abramu alikuwa mtu wa miaka sabini na mitano alipotoka Harani." Kufikia wakati huo Ibrahimu hakuwa kijana, alikuwa amejijenga, tena alikuwa tajiri, lakini Ibrahimu alipoisikia sauti ya Mwenyezi Mungu alitii pasipo shaka lo lote. Ibrahimu alikuwa hajaambiwa mahali ambako angepaswa kwenda ila aliambiwa afungashe mizigo na kuondoka, akiwa na imani kabisa kwamba Mwenyezi Mungu angemwongoza. Angalia, Ibrahimu alikuza uhusiano wake na Mwenyezi Mungu, alifahamu kwamba njia yake ni bora kuliko zote, hata wakati ule alipokosa kufahamu kikamilifu kwa nini mambo yawe vile, aliliamini tu Neno la Mwenyezi Mungu na kutii matakwa yake. Sisi nasi pia, tungetenda vema kuwa na utii ule ule aliokuwa nao Ibrahimu kwa Mwenyezi Mungu.

### *Ibrahimu aitwa kuchinja kafara*

Kurani Tukufu yatuambia kwamba Musa alipewa Maandiko (Taurati) na kanuni ya kupambanua baina ya yaliyo ya haki na yasiyokuwa ya haki. Sura 2:53 Al Baqarah "Na (kumbukeni) Tulipompa Musa Kitabu (kilichokusanya kila wanayoyahitajia) na cha kupambanua baina ya yaliyo ya haki na yasiyokuwa ya haki ili mpate kuongoka." Katika Mwanzo (Taurati) kimeandikwa kisa chote cha Ibrahimu. Katika Sura ya 22 ya Mwanzo kimeandikwa kisa cha Ibrahimu alivyotakiwa kumchinja na kumtoa sadaka mwanawe. Kinatufunulia jinsi yalivyotokea mambo hayo. Lakini, je, kisa hiki ni cha maana kwetu? Twaambiwa katika Sura 26:69 kwamba sisi tunapaswa 'kusomea' kisa chake Ibrahimu. Nabii Muhammad alijua kwamba kisa hiki kingekuwa cha maana sana kwetu kukijua, kwa maana kinalo fundisho la kutufundisha sisi. Hivyo twataka kutoa kisa chote hapa. 026:069 Ash-Shuaraa

"Na wasomee habari za (Nabii) Ibrahimu." Katika Mwanzo 22:2 (Taurati) imeandikwa … "akasema [Mwenyezi Mungu], Umchukue mwanao, mwana wako wa pekee" … halafu yanafuata maneno haya machungu mno … "umpendaye … ukaende zako mpaka nchi ya Moria, ukamtoe sadaka ya kuteketezwa huko juu ya mlima mmojawapo nitakaokuambia."

Mwenyezi Mungu alipomtaka Ibrahimu amtoe sadaka mwanawe, Ibrahimu alitii bila swali. Kisa hiki pia kimeandikwa kwa kifupi katika As-Saaffat Sura 037:102-107. Hii isingekuwa kazi rahisi kwa Ibrahimu kutekeleza! Moyo wake wenye huruma bila shaka uliumia vibaya sana zaidi ya maelezo yo yote yawezayo kutolewa. Lakini Neno kutoka kwa Mwenyezi Mungu lilikuwa limetolewa, amri ile ilisikika kwa wazi kabisa moyoni mwake na Ibrahimu alikuwa na mazoea ya kuongea na Mwenyezi Mungu. Uhusiano ulikuwa umekuzwa baina ya Mwenyezi Mungu na yeye mwenyewe kiasi kwamba aliifahamu sauti ya Mwenyezi Mungu alipoisikia. Na upendo aliokuwa nao Ibrahimu kwa Mwenyezi Mungu ulikuwa ni wa kutii alipoisikia sauti yake, hata kama alikuwa haelewi kikamilifu sababu yake ni nini.

### *Ibrahimu aitwa 'Hanif'*

Ibrahimu anafikiriwa kuwa yeye ni 'Hanif' miongoni mwa wale walio wanyofu wa moyo kweli kweli na waliojitoa kumtumikia Mwenyezi Mungu. Waitwao 'Hanif' ni wale walio safi sana katika dini yao kwa Mwenyezi Mungu. Katika Mwanzo 22:3 tunayo maelezo kwa nini Ibrahimu anafikiriwa kuwa ni 'Hanif'. Baada ya Ibrahimu kupewa ujumbe ule, maelezo yanasema … "Ibrahimu akaondoka alfajiri, akatandika punda wake, akachukua vijana wawili pamoja naye, na Isaka mwanawe, akachanja kuni kwa ajili ya hiyo sadaka ya kuteketezwa, akaondoka, akaenda mpaka mahali alipoambiwa na Mungu." Hilo ndilo linalomfanya Ibrahimu kuwa miongoni mwa 'Hanif'. Ibrahimu aliposikia sauti ya Mwenyezi Mungu alitii na kufanya kile alichotakiwa kufanya. Je, hivi ni kweli leo kwamba wale wanaoitii sauti ya Mwenyezi Mungu, yaani, wale wanaomtii bila swali wamo pia miongoni mwa 'Hanif'?

### *Ibrahimu aitwa kwenda Mlima wa Moria*

Kazi hii ambayo Mwenyezi Mungu alikuwa amemtaka Ibrahimu kuifanya ilikuwa si mchezo. Twaweza kuona kwamba ilichukua siku tatu kwenda nchi ya Moria. Bila shaka zilikuwa siku ndefu za maumivu makali akijua kwamba huenda angerudi peke yake kutoka mahali pale pa kutolea sadaka. Twashangaa iwapo Ibrahimu alipata pumziko lo lote wakati wa usiku wengine walipolala usingizi. Kwa hakika Ibrahimu alishindana na Mungu kila usiku katika maombi juu ya jambo hilo. Twaendelea kusoma: (Taurati) Mwanzo 22:4 "Siku ya tatu Ibrahimu akainua macho yake, akapaona mahali pakali mbali. Ibrahimu akawaambia vijana wake, Kaeni ninyi hapa pamoja na punda, na mimi na kijana tutakwenda kule, tukaabudu, na kuwarudia tena."

Hakuna mtu aliyepaswa kushuhudia tukio hili mbele ya Mwenyezi Mungu, zaidi ya yule baba na mwanawe. Hivyo "Basi Ibrahimu akazitwaa kuni za hiyo sadaka, akamtwika Isaka mwanawe; akatwaa moto na kisu mkononi mwake, wakaenda wote wawili pamoja." Fungu la 6. Kabla ya muda mrefu kupita mwana wa Ibrahimu alisema hivi … "Babaangu … Tazama! moto upo, na kuni zipo, lakini yuko wapi mwana-kondoo kwa sadaka ya kuteketezwa? Ibrahimu akasema, Mungu atajipatia mwana-kondoo kwa hiyo sadaka, mwanangu. Basi wakaendelea wote wawili pamoja."

Wakafika mahali pale, madhabahu ikajengwa, kuni zikawekwa juu ya madhabahu, na ndipo habari ilipoelezwa waziwazi kwa mwanawe Ibrahimu ya kwamba yeye ndiye angekuwa ile sadaka. Mwanawe alitii kile Mwenyezi Mungu alichokuwa amemtaka Ibrahimu kufanya, na yule mwana akawekwa juu ya madhabahu. Huyu alikuwa ndiye yule mwana mpendwa wa Ibrahimu katika uzee wake. Ndipo Ibrahimu alipoinua juu mkono wake wenye kisu … mkono wake ule ukazuiwa…

Ibrahimu alipokuwa karibu kumchinja mwanawe, sauti ikasikika … "Ibrahimu, Ibrahimu,' naye akasema, "Mimi hapa". Mwanzo 22:11. Inaendelea kwenye mafungu 12-13. "[Mwenyezi Mungu] akasema, Usimnyoshee kijana mkono wako, wala usimtendee neno; kwa maana sasa ninajua ya kuwa unamcha [Mwenyezi] Mungu, iwapo hukunizuilia mwanao, mwanao pekee. Ibrahimu akainua macho yake, akaangalia, na tazama, kondoo mume yuko nyuma yake, amenaswa

pembe zake katika kichaka. Basi Ibrahimu akaenda akamtwaa huyo kondoo, akamtoa awe sadaka ya kuteketezwa badala ya mwanawe."

### *Mwanawe Ibrahimu Akombolewa*

Ni kwa njia gani mwanawe Ibrahimu alikombolewa? Kurani Tukufu yasema kwamba mwanawe alikombolewa kwa sadaka ya kuchinjwa tukufu! Sura 37:107

"Basi tukamkomboa kwa mnyama wa kuchinjwa mtukufu." Hatuna budi kujiuliza, je, kondoo yule mume aliyenaswa katika kichaka, alikuwa "Mnyama wa Kuchinjwa Mtukufu" kweli? Au

kuna habari zaidi kwa kisa hiki? Je, ingewezekana kwamba yule kondoo mume aliyenaswa katika kichaka ambaye alitolewa na Mwenyezi Mungu alikuwa akidokeza ile "Kafara Kuu"? Je, ile ilimwakilisha Yeye ambaye Mwenyezi Mungu angemteremsha kuwa sadaka ya dhambi kwa ulimwengu wote? Kwa maana yake mwanawe Ibrahimu aliwakilisha wanadamu wote. Sisi sote tungekufa milele, kama matokeo ya dhambi, lakini twaweza kuishi, kwa sababu ya mwana-kondoo mume aliyetolewa sadaka badala yetu, yaani, ukombozi ule uliotolewa na Mwenyezi Mungu. Jina lake lilikuwa Masihi Isa, Kristo Yesu. Aliteremshwa kutoka kwa Mwenyezi Mungu kuwa upatanisho kwa ajili ya wanadamu. Mwanadamu alikuwa ameanguka, lakini Mwenyezi Mungu angeweza kutoa ufumbuzi. Jamii yenye dhambi ilipaswa kukombolewa kwa kafara tukufu sana ya Yeye aliyeteremshwa kutoka kwa Mwenyezi Mungu.

### *Ibrahimu aitwa Mbarikiwa na Mwenyezi Mungu*

Kwa kuwa Ibrahimu aliitii sauti ya Mwenyezi Mungu katika jambo hili, maelezo yaliyo katika Mwanzo 22:17-18 (Taurati) yanamwita Ibrahimu kuwa amebarikiwa na Mwenyezi Mungu. Walakini si Ibrahimu peke yake aliyepaswa kubarikiwa, bali pia uzao wa Ibrahimu, hata mataifa yote ya dunia. "Katika kubariki nitakubariki, na katika kuzidisha nitauzidisha uzao wako kama nyota za mbinguni, na kama mchanga ulioko pwani; … na katika uzao wako mataifa yote ya dunia watajibarikia; kwa sababu umetii sauti yangu."

Katika Mwanzo 26:5 twaambiwa tena sababu iliyomfanya Ibrahimu abarikiwe na Mwenyezi Mungu … "Kwa sababu Ibrahimu alisikia sauti yangu, akayahifadhi maagizo yangu, na amri zangu, na hukumu zangu, na sheria zangu." Baadhi ya watu watatoa hoja kwamba Amri Kumi zilikuwa hazijatolewa hadi wakati wa Musa pale Sinai, yaani kipindi kirefu baada ya Ibrahimu, lakini kisa hiki kinathibitisha milele ukweli kwamba hata Ibrahimu alizitii Amri Kumi za Mwenyezi Mungu kwa maana imeandikwa kwamba Ibrahimu alizitii Amri zake Mwenyezi Mungu.

Tukitaka kupata baraka za Mwenyezi Mungu, sharti tupende kwa moyo kutoa utii wetu kwa Neno la Mwenyezi Mungu na kwa Amri zake, kwa njia ile ile aliyotii Ibrahimu. Kwa hakika kabisa, nasi pia tutabarikiwa na Mwenyezi Mungu.

Aya zote katika Maandiko ya Agano la Kale (Taurati) zisemazo juu ya kuchinja sadaka za wanyama zilikusudiwa kumwongoza mtu kutazama mbele kwenye ile 'Kafara Kuu (Tukufu)', ya 'Thamani Kuu' ambayo ingeteremshwa kutoka kwa Mwenyezi Mungu. Lakini hatimaye Masihi Isa alipokuja, ni wachache mno waliouelewa utume wake. Wachache mno waliamini kwamba huyu alikuwa ndiye Masihi kweli kweli, yaani, yule Sadaka ya Dhambi, Mkombozi, Mwokozi wa Ulimwengu ulioanguka dhambini.

Kwa nini Mwenyezi Mungu alimtaka Ibrahimu aende kwenye Mlima wa Moria? Huu ulikuwa ni mlima ule ule ambao juu yake baadaye hekalu lilijengwa, lakini pia ni mahali pale pale hasa ambapo miaka mingi baadaye, Masihi Isa, alitoa maisha yake kuwa kafara kwa ajili ya jamii yote ya wanadamu. Ilikuwa ni juu ya mlima ule ule ambapo karne nyingi kabla yake mkono wa Ibrahimu ulizuiwa ili kumwokoa mwanawe, lakini safari hii mkono wa Mwenyezi Mungu mwenyewe haukuzuiwa, na Yeye (Masihi Isa) aliyekuwa karibu sana na Mwenyezi Mungu akachinjwa kama sadaka kwa ajili ya binadamu wote. Uhai wake Masihi Isa ulitolewa kwa ajili yetu. Yaliyompata Ibrahimu kwa mwanawe, lilikuwa ni fumbo linaloonesha yale ambayo yangekuja baadaye. Katika siku zake Ibrahimu, ukombozi ulipatikana, yaani, yule kondoo mume kichakani. Katika Injili, inasema … "… Mwana wa Adamu … [alikuja] kutoa nafsi yake iwe fidia ya wengi" (Mathayo 20:28).

Hapo kale, wenye hekima kutoka Mashariki walijua kwamba ukombozi ungekuja kwa ajili ya wanadamu. Katika Vitabu Vitakatifu twasoma haya yafuatayo: … "Mwokoe asishuke shimoni; Mimi nimeuona ukombozi" Ayubu 33:24.

Ukombozi ni gharama inayolipwa kwa ajili ya mwenye dhambi ili apate kusamehewa dhambi zake. "Mshahara wa dhambi ni mauti', na ilimpasa mtu fulani kulipa gharama hiyo kwa ajili ya mwanadamu, vinginevyo, yeye kwa hakika angetazamia tu kushuka shimoni [kwenye maangamizi], imeandikwa katika Injili, kwamba Mwenyezi Mungu alitoa sadaka ya dhambi, yaani, ukombozi … Waebrania 10:12 "Lakini huyu (Masihi Isa), alipokwisha kutoa kwa ajili ya dhambi dhabihu moja idumuyo hata milele, aliketi mkono wa kuume wa [Mwenyezi] Mungu". 1 Yohana 2: 2 "Naye (Masihi Isa) ndiye kipatanisho kwa dhambi zetu; wala si kwa dhambi zetu tu, bali na kwa dhambi za ulimwengu wote."

Mpendwa rafiki wa Mwenyezi Mungu, je, hutaipokea sadaka hii ya dhambi, yaani, ukombozi huu ulioteremshwa kutoka kwa Mwenyezi Mungu kwa ajili yako? Ni kwa ajili yako Mwenyezi Mungu alimteremsha Masihi Isa, kama "Mnyama wa Kuchinjwa Mtukufu". Ameteremshwa kwako wewe na kwangu mimi, kama Mwokozi wetu anayetutoa kutoka dhambini. Tafadhali ipokee leo dhabihu hii iliyotolewa kwa neema kwa ajili yako!

### 'Waliopewa Kitabu'!

Kurani Tukufu huelekeza kidole chake kwenye kundi lile liitwalo "Waliopewa Kitabu". Msomaji anaombwa asome Sura 3:113-115. Aali Imran.

003:113 "Wao (Waliopewa Kitabu) si wote sawa. Katika (hao) Waliopewa Kitabu wamo watu waliotengenea - wanasoma Aya za Mwenyezi Mungu nyakati za usiku, na pia wanasujudu (yaani wamesilimu)."

003:114 "Wanamwamini Mwenyezi Mungu na Siku ya Mwisho, na wanaamrisha mema na wanakataza maovu na wanayaendea mbio mambo mema. Na hao ndio miongoni mwa hao watendao mema (kweli kweli)."

003:115 "Na heri yo yote watakayoifanya hawatakanushiwa (thawabu zake). Na Mwenyezi Mungu anawajua wanaomcha (wakajiepusha na makatazo yake na wakafanya maamrisho yake)."

Watu hao wanajulikana kama 'Wakristo'. Hao wanaitwa 'Waliopewa Kitabu' (Maandiko ya Biblia). Lakini miongoni mwao limo kundi la pekee. Kurani Tukufu yasema kwamba ipo tofauti kati ya hao 'Wakristo' na ya kwamba 'si wote sawa.'

Je, kundi hilo la pekee ni akina nani ambao Nabii Muhammad (jina lake na liheshimiwe) alivuta mawazo ya watu kuelekea kwao kwa namna ya ajabu kama hiyo, akisema wao ni 'miongoni mwa hao watendao mema kweli kweli'!

Hebu zingatia tabia zinazolitambulisha kundi hili la pekee kutoka katika Sura 3:113-115

1. si (Wakristo) wote sawa
2. katika (hao) waliopewa Kitabu wamo watu waliotengenea
3. wanasoma Aya za Mwenyezi Mungu
4. wanasujudu
5. wanamwamini Mwenyezi Mungu na Siku ya Mwisho
6. wanaamrisha mema [wanafundisha kwa mamlaka yaliyo ya haki]
7. wanakataza maovu
8. wanayaendea mbio mambo mema [wanajitahidi kufanya yale yenye sifa njema]
9. hao ndio miongoni mwa hao watendao mema kweli kweli
10. na heri yo yote watakayoifanya hawatakanushiwa. [Mwenyezi Mungu anawajua]

Kurani Tukufu yasema hivi kuhusu kundi hilo la pekee, kwamba hao "ndio miongoni mwa hao watendao mema kweli kweli". Iwapo hao ni miongoni mwa hao watendao mema kweli kweli, basi yale wayasadikiyo hayana budi kuwa ndiyo kweli yenyewe. Kama Mwenyezi Mungu anawaita kuwa wamo miongoni

mwa hao watendao mema kweli kweli, basi, sisi hatuthubutu kabisa kuwakosoa. Lakini je! si afadhali sisi pia tungeweza kujifunza kitu kwao? Twaona ya kwamba watu hao wa pekee wanakishikilia kile 'Kitabu' (Maandiko ya Biblia) ambacho Nabii Muhammad kwa makusudi mazima alituelekeza sisi kwenye [Kitabu] hicho katika Kurani Tukufu (Al Maidah) Sura 5:46 … "Na tukawafundisha (Mitume hiyo) Isa bin Maryamu kuyahakikisha yaliyokuwa kabla yake katika Taurati, na tukampa Injili iliyomo ndani yake uongozi na nuru na isadikishayo yaliyokuwa kabla yake katika Taurati, na uongozi na mauidha kwa wamchao (Mwenyezi Mungu)."

Watu hao wanasadiki kwamba ni jukumu lao kujitoa kabisa kwa Mwenyezi Mungu pasipo kuzuia kitu, kuwa na utii kwake usio na swali. Watu hao wana maadili ya kiwango cha juu, ambayo yamejengwa juu ya Maandiko ya Biblia. Wanamheshimu Mwenyezi Mungu kuwa ndiye Mkuu kuliko wote, tena hawana mshirika ye yote (kama vile Maryamu au wale wengine waitwao watakatifu wanaoabudiwa) ambaye wanamfungamanisha na huyo Mungu kama Wakristo wengi sana wafanyavyo. Katika Injili maneno haya hunenwa: Yakobo 2:19 "Wewe waamini ya kuwa Mungu ni mmoja; watenda vema." … na katika Marko (Masihi Isa) Kristo Mwenyewe alisema… "Bwana Mungu wetu ni Bwana mmoja". Watu hao hawazisujudu sanamu katika ibada yao kama wafanyavyo Wakristo wengi sana. Wanasadiki kwamba kuabudu sanamu au mifano iwayo yote kumekatazwa kabisa na Mwenyezi Mungu, kama ilivyoandikwa katika Taurati, Kutoka 20:4-5 "Usijifanyie sanamu ya kuchonga, wala mfano wa kitu cho chote kilicho juu mbinguni, wala kilicho chini duniani, wala kilicho majini chini ya dunia. Usivisujudie wala kuvitumikia". Watu hao wanajua kwamba kuabudu hiyo mifano na sanamu kumekatazwa kabisa katika Maandiko ya Biblia.

Yaendelea [Kurani Tukufu] kusema kwamba watu hao katika ibada yao kwa Mwenyezi Mungu 'wanasujudu', yaani, wanapiga magoti mbele zake Mwenyezi Mungu kama Daudi alivyoandika katika Zaburi (Taurati), Zaburi 95:6 "Njoni, tuabudu, tusujudu, tupige magoti mbele za BWANA aliyetuumba."

Katika Sura 3:114 inatuambia sisi kwamba 'wanakataza maovu'. 'Hao' miongoni mwa "wao Waliopewa Kitabu" wanakataza kula vyakula najisi (haramu) kama 'Nyama ya nguruwe'. (Taurati) Mambo ya Walawi 11:7 "Na nguruwe, … yeye ni najisi kwenu." Wanakataza matumizi ya vileo, tumbako, na vitu vingine vinavyodhuru (haramu) afya ya mwili na kuuangamiza. Wanaziheshimu Amri Kumi za Mwenyezi Mungu kama zilivyoandikwa katika (Taurati) Kutoka 20. Watu hao wanasadiki kwamba

tunaishi katika "Siku za Mwisho" za historia ya dunia hii…

### *Waadventista Wasabato*

Je! kundi hilo la pekee la "Waliopewa Kitabu" ambao juu yao Kurani Tukufu inaongea sifa nyingi sana ni akina nani? Lipo kundi la watu miongoni mwa "Waliopewa Kitabu" lijulikanalo kama: "Waadventista Wasabato (Seventh.Day Adventists)". Hapa chini yapo maelezo mafupi kuhusu yale wanayoyaamini. Linganisha yale wayaaminiyo na kuelewa iwapo yanapatana na maelezo yaliyotolewa katika Sura 3:113-115? Je, hao ndilo lile kundi la "si wote" miongoni mwa waliopewa kitabu, yaani, ambao wamo miongoni mwa hao watendao mema kweli kweli?

Waadventista Wasabato wanaamini:

1. Kwamba wanamtumikia [Mwenyezi] Mungu Mmoja na kwamba hawamhesabii Mwenyezi Mungu kuwa anao washirika kama vile Bikira Maria na wengine waitwao watakatifu wanaoabudiwa. Injili Yakobo 2:19 'Wewe waamini kuwa Mungu ni mmoja; watenda vema..'…

2. Wanampa Mwenyezi Mungu roho zao zote. (Injili) Luka 10:27 'Akajibu akasema, Mpende Bwana Mungu wako kwa moyo wako wote, na kwa roho yako yote, na kwa nguvu zako zote, na kwa akili zako zote; na jirani yako kama nafsi yako.'

3. Hawamtumikii Mwenyezi Mungu kwa njia ya sanamu na mifano, vitu hivyo vimekatazwa kabisa. Kutoka 20:4-6 "Usijifanyie sanamu ya kuchonga, wala mfano wa kitu cho chote …Usivisujudie wala kuvitumikia; kwa kuwa mimi, BWANA, Mungu wako [Mwenyezi Mungu], ni Mungu mwenye wivu…"

4. Wanaamini kwamba siku ya saba (siku ya mwisho) ya juma ni siku bora kuliko zote. Wanaiheshimu siku ile kwa kumfanyia ibada Muumbaji [Mwenyezi Mungu]. Ni siku ile iitwayo "Sabt" ambayo ina maana ya 'pasipo kazi' katika lugha ya Kiarabu. Wanazifuata amri zote za Mwenyezi Mungu kama zilivyotolewa katika (Taurati) Kutoka 20:8-11 'Ikumbuke siku ya Sabato uitakase. Siku sita fanya kazi, utende mambo yako yote; lakini siku ya saba ni Sabato ya BWANA, Mungu wako, siku hiyo usifanye kazi yo yote, wewe, wala mwana wako, wala binti yako, wala mtumwa wako, wala mjakazi wako, wala mnyama wako wa kufuga, wala mgeni aliye ndani ya malango yako. Maana, kwa siku sita BWANA alifanya mbingu, na nchi, na bahari, na vyote vilivyomo, akastarehe siku ya saba; kwa hiyo BWANA akaibarikia siku ya Sabato akaitakasa.' Wao wanaamini kwamba Mwenyezi Mungu ndiye Muumbaji na ya kwamba aliiumba dunia na vyote vilivyomo ndani yake kwa siku sita na kupumzika siku ya saba.

### *Sura 10:3*

10:003 'Bila shaka Mola wenu ni Mwenyezi Mungu ambaye ameziumba mbingu na ardhi katika siku sita. Kisha akatawala juu ya Arshi yake [Kiti chake cha enzi]. Yeye ndiye anayepitisha mambo yote. Hakuna Muombezi ila baada ya idhini yake (Mungu). Huyu ndiye Mwenyezi Mungu, Mola wenu. Basi Muabuduni Yeye. Je! hamkumbuki (kuwa hayo mliyo nayo siyo mambo ya haki)? Sura 10:003 Yunus

Hebu fikiria tu jinsi wewe mwenyewe uwezavyo kuitumia siku nzima, yaani, siku ile ya mwisho, (ya saba) ya juma, siku bora kuliko zote, kwa ajili ya kujitoa kabisa kwake Mwenyezi Mungu! Kuitumia siku hiyo kumwabudu na kumsifu Mwenyezi Mungu, kushirikiana na kutiana moyo kila mmoja na mwenzake. Kuweka kando biashara yote na mambo ya ulimwengu huu, mambo yote yanayosambaratisha mawazo yako, na kuichukua familia yako kwenda kumwabudu Mwenyezi Mungu na kutumia muda huo pamoja na kila mmoja pengine kwa kutembea kimya kimya kuangalia viumbe vya asili. Kweli huu ndio mbaraka ambao wachache mno huutambua. Je, huo usingejumuisha kumpenda Mwenyezi Mungu kwa moyo wako wote?

Jambo la mwisho, watu hao ni wafuasi wa Masihi Isa (Kristo aitwaye Masihi). Sura 3:055

3:055 (Kumbukeni) Mwenyezi Mungu aliposema: 'Ewe Isa! Mimi nitakutimizia muda wako wa kuishi (hawatakuua hao maadui). Na nitakuleta kwangu, na nitakutakasa na wale waliokufuru, (hawataweza kukudhuru) na nitawaweka wale waliokufuata, juu ya wale waliokufuru, mpaka siku ya Kiyama. Kisha marejeo yenu yatakuwa kwangu, nikuhukumuni katika yale mliyokuwa mkihitilafiana.' 3:055 Aali Imran. Msomaji anaombwa ajifunze juu ya Waadventista Wasabato.

### 'Nabii kama Musa'…

Mjadala mwingi umehusisha aya inayopatikana katika Maandiko ya Biblia ambayo ndiyo kichwa cha somo letu leo. Wasomi wengi wanafahamu kuwa aya hii inaonesha mbele hadi kwa Nabii Muhammad anayeheshimiwa!

Taurati Kumbukumbu la Torati 18:15,18 "BWANA, Mungu [Mwenyezi Mungu] wako, atakuondokeshea nabii miongoni mwa ndugu zake kama nilivyo mimi; msikilizeni yeye. Mimi [Mwenyezi Mungu] nitawaondokeshea nabii miongoni mwa ndugu zao mfano wako wewe, nami nitatia maneno yangu kinywani mwake, naye atawaambia yote nitakayomwamuru."

Wasomi wenye akili nyingi hutumia sana aya hizo juu na kwa kujiamini wanasema, huyo ni yule Nabii anayeheshimiwa anayetajwa hapa katika 'Taurati' Kumbukumbu la Torati katika Maandiko ya Agano la Kale. Kwa mtazamo wa kawaida inaonekana hakika kwamba hilo laweza kuwa la kweli. Hata hivyo, twahitaji kuyachunguza zaidi madai

haya. Wako wengi wanaotoa madai kwa sababu yanapendeza, lakini ngoja, je hakuna baadhi ya wasomi wanaodai kwamba Maandiko ya Biblia yamechafuliwa? Wanasema kwamba yamekuwa ya uongo kiasi cha kutoweza kuyaamini. Basi mbona wasomi hao Waislamu wadondoe kutoka katika chanzo wanachojisikia kuwa kimechafuliwa? Hivi wanajuaje kwamba aya zizo hizo wanazodondoa zenyewe hazimo miongoni mwa zile zilizochafuliwa? Yote hayo ni utata mtupu au huonekana hivyo, isipokuwa kama sisi twatafuta yaliyo kweli mbali na yale ya uongo.

005.048 "Na tumekuteremshia Kitabu kwa (ajili ya kubainisha) haki, kinachosadikisha vitabu vilivyokuwa kabla yake, na kuvihukumia (kama haya ndivyo yalivyoharibiwa au ndivyo yalivyosalimika). Basi wahukumu baina yao kwa yale aliyoyateremsha Mwenyezi Mungu, wala usifuate matamanio yao kwa kuacha haki iliyokufikia. Na kila (umma) katika ninyi (binadamu) tumeujaalia sharia yake na njia yake. Na kama Mwenyezi Mungu angalitaka angekufanyeni kundi moja (la kufuata sharia moja), lakini anataka kukujaribuni kwa hayo aliyokupeni. Basi shindaneni kuyafikilia mambo ya heri. Ninyi nyote marudio yenu ni kwa Mwenyezi Mungu; naye atakwambieni (yote) yale mliyokuwa mkihitilafiana."

Al-Qur'an, 005.048 (Al Maidah [Meza, Meza Iliyoandaliwa]).

Kurani Tukufu inaeleza wazi kabisa ya kwamba Mwenyezi Mungu ateremshaye hayo Maandiko pia ndiye ayalindaye. Mwenyezi Mungu pia atatuonesha sisi yaliyo ya kweli. Alikuwa ameiteremsha Taurati kwa njia ya Musa, Zaburi kwa njia ya Daudi na Injili kwa njia ya Masihi Isa. Awezaje mwanadamu anayekufa kuthibitisha kwamba kile kilichoteremshwa wakati uliopita sasa kimechafuliwa au kimechanganywa na uongo? Na ni nani aliyeko huko ambaye yuko juu ya Mwenyezi Mungu, na ni nani angeweza kufanya jambo kama hilo? Huenda ziko aya nyingi katika Vitabu Vitakatifu ambazo kwa msomaji wa juu juu tu zinaweza kumpotosha. Lakini kwa dua inayotolewa kwa dhati na saumu maneno hayo yanaweza kueleweka. Kumbukeni ya kwamba mambo ya kiroho hutambuliwa kwa mambo ya kiroho.

Injili Mathayo 11:25 "Wakati ule Yesu [Masihi Isa] akajibu, akasema, Nakushukuru, Baba, Bwana wa mbingu na nchi, kwa kuwa mambo haya [Mwenyezi Mungu] uliwaficha wenye hekima na akili, ukawafunulia watoto wachanga [wajifunzao

kwa unyenyekevu]."

Tusipokuwa miongoni mwa wajifunzao kwa unyenyekevu na endapo sisi tuna hekima machoni petu wenyewe, basi, tutakosa kuelewa mambo ambayo mbingu inajaribu kutufunulia. Kwa hiyo ni muhimu kwamba tuombe kwa unyenyekevu na tupewe roho ya mwanafunzi aliye tayari kujifunza. Ni nani kati yetu awezaye kumfundisha Mwenyezi Mungu? Nani awezaye kujua mengi kuliko yeye? Tena katika Injili tunaambiwa yafuatayo…

Injili 1 Wakorintho 2:14 "Basi mwanadamu wa tabia ya asili hayapokei mambo ya Roho wa Mungu; maana kwake huyo ni upuzi, wala hawezi kuyafahamu, kwa kuwa yatambulikana kwa jinsi ya rohoni."

Kwa hakika lingekuwa tusi la kutisha kwa Mwenyezi Mungu, ambaye bila shaka lo lote ameteremsha maneno yaliyotangulia kwa ajili ya wanadamu, hata kule kudokeza tu kwamba yeye, Mwenyezi Mungu hawezi kulilinda neno lake katika ukamilifu wake mbali na watu wenye mawazo maovu [ni kufuru]. Je, Mwenyezi Mungu hana nguvu kuliko Majini (malaika walioanguka) au zaidi ya wale walioathiriwa nayo? Basi yatupasa kuwa miongoni mwa wale waaminio na tusiwe na wale wenye mashaka. Kwa maana mwenye mashaka aliyethibitika hivyo hawezi kupokea kitu cho chote kutoka kwa Mwenyezi Mungu isipokuwa hasara ya kupotea milele.

Kumbukeni Mwenyezi Mungu hashindwi kamwe kutimiza ahadi yake…

Sura 3.009

بِسا ّنلا ُعِماَج َكّ َنِا اَن ّبَ رَ
هَّللَا ّنَ ِاِهيِف َبْيَر ال ٍمْوَيِل
داَعيِمْلا ُفِلْخُي ال

003.009 "Mola wetu! Wewe ndiwe Mkusanyaji wa watu katika Siku isiyo na shaka ndani yake. Hakika Mwenyezi Mungu havunji miadi." (Aali Imran [Familia ya Imran])

Mwenyezi Mungu ameahidi kwamba yale anayoyateremsha atayalinda yasiharibiwe.

Sura 15:09

رَكْ ّذِلا انَلْ ّزَنَ نُحْنَ ا ّنَ اِ
نَوُظِفاَحَلَ هُلَ ا ّنَ اِوَ

"Hakika Sisi ndio tulioteremsha mauidha haya, na hakika Sisi ndio tutakaoyalinda (yasiharibiwe).

Al-Qur'an, 015.009 Al Hijr

Wapo wale walio na shaka kuhusu yale aliyoyafunua Mwenyezi Mungu. Hapo ndipo Nabii Muhammad anatuambia kwamba kama tuna shaka, basi tuwaulize wale waliopewa kile Kitabu (Maandiko ya Biblia) kabla yetu. Yunus 10:94

ا ّمِم ٍّكَش يِف َتْنُك ْنِاَف
لَأْسا َف  َكْيَل ِا  ا َنْل َزْنَأ
بَاتَكِلْا نَوُءَرْقَي نَيِذ ّلَا
ّقَحلْا َكَءاَج ْدَقَل َكِلْبَق ْنِم
نَمِ ّنَنوُكَت الَف كَّبَر نْم
نَيِرَتْمُمْلا

010.094 "Na kama unayo shaka juu ya hayo tuliyokuteremshia, basi waulize wale wasomao vitabu kabla yako (Mayahudi na Manasara wale waliosilimu). Kwa yakini haki imekwisha kukujia kutoka kwa Mola wako, kwa hiyo usiwe miongoni mwa wanaofanya shaka.

Al-Qur'an, 010.094 (Yunus [Yona])

Leo twataka kuwauliza wale ambao wamekuwa wakikisoma kile Kitabu, yaani, Maandiko ya Biblia, juu ya nani aliyenenwa habari zake katika Taurati Kumbukumbu la Torati 18:18 "Mimi [Mwenyezi Mungu] nitawaondokeshea nabii miongoni mwa ndugu zao mfano wako wewe."…

Injili Matendo 3:20-22 "[Mwenyezi Mungu] apate kumtuma Kristo Yesu [Masihi Isa], mliyewekewa tangu zamani; ambaye ilimpasa kupokewa mbinguni hata zije zamani za kufanywa upya vitu vyote, zilizonenwa na [Mwenyezi] Mungu kwa kinywa cha manabii wake watakatifu tokea mwanzo wa ulimwengu. Kwa maana Musa kweli alisema ya kwamba, Bwana Mungu wenu atawainulieni nabii, katika ndugu zenu, kama mimi; msikieni yeye katika mambo yote atakayonena nanyi."

Inakuwa wazi kabisa katika Injili, ya kwamba Masihi Isa angetumwa ambaye angekuwa kama nabii Musa. Ilikuwa ikimtaja Isa wala si mtu mwingine.

Twawezaje kuwa na hakika? Endapo tu sisi hatukumpata kwa mara yetu ya kwanza, kwa rehema habari hiyo inarudiwa pamoja na maelezo ya nyongeza yanayotuambia mtu huyo ni nani.

Injili Matendo 7:37-38 'Musa huyo ndiye aliyewaambia Waisraeli, Bwana Mungu [Mwenyezi Mungu] wenu atawainulieni nabii, katika ndugu zenu, kama mimi [Musa]; msikieni yeye. Yeye ndiye [Isa] aliyekuwa katika kanisa [umma wa walioamini] jangwani pamoja na yule malaika aliyesema naye katika mlima wa Sinai, tena pamoja na baba zetu; ndiye aliyepokea maneno ya uzima atupe sisi."

Injili Matendo 7:52 Kwa maneno yanayoeleweka wazi mjumbe yule Stefano aliwaambia Wayahudi wale wa zamani… "Ni yupi katika manabii ambaye baba zenu hawakumwudhi? Nao waliwaua wale waliotabiri habari za kuja kwake yule Mwenye Haki [Masihi Isa]; ambaye ninyi sasa mmekuwa wasaliti wake, mkamwua."

Inatuambia sisi kwamba mtu huyu ambaye angekuwa kama nabii Musa, angekuwa ni mtu yule yule aliyekuwa pamoja na wale waliotoka Misri na akawa pamoja na wale waliokuwa jangwani wakati sauti ya Mwenyezi Mungu iliposikika kutoka juu ya Mlima Sinai. Alikuwa ni Masihi Isa aliyekuwa pale. Hilo liko dhahiri kabisa katika aya hii. Hakuwa yule Nabii Muhammad Anayeheshimiwa ambaye alikuwa kule jangwani, bali ni Masihi Isa. Basi sasa sisi tunafahamu ya kwamba Masihi Isa ndiye mtu yule aliyetajwa katika aya ya Kumbukumbu la Torati 18:15 & 18 na wala si mtume Muhammad. Kama tukiwa na subira na kuendelea kuuliza tutang'amua kwamba siku zote Maandiko yanajitafsiri au kujifafanua yenyewe.

Alikuwa ni Isa ambaye alipaswa kuwaongoza wale walioamini kutoka utumwani kama alivyofanya nabii Musa. Musa aliwaongoza Waisraeli kutoka utumwani Misri kwenda kwenye uhuru. Walipita jangwani. Musa alistahimili mapambano mengi, wakati mwingine wale waliokuwa wamewekwa huru walitaka kumwua

Musa kwa sababu walikosa subira na walikuwa wamechoka. Hivyo ndivyo ilivyo hata kwa Masihi Isa, kwa njia iyo hiyo anawaongoza watu, wale wanaoamini, kutoka katika jangwa la dhambi na giza na kuwaingiza katika uhuru ufurahishao wa ile kweli. Isa anawaongoza watu kwenda katika nchi ile ya ahadi, yaani, mbinguni, kwa njia ambayo karibu inafanana sana na vile Musa alivyofanya katika kuwaongoza wana wa Israeli kutoka Misri kwenda Kanaani, nchi ile ya ahadi. Sisi hatutazamii kwenda Kanaani ya duniani bali ile ya Mbinguni. Nchi ile ni nzuri ambayo ndani yake amani inatawala milele na ambako wale wanaotamani amani watakuwako. Watu wenye amani waipendao kweli watakuwa kule. Yaani, watu wale ambao maisha yao yamebadilishwa na yule Mmoja ambaye amekuwa akiwaongoza njiani wakati wote. Hebu wewe na mimi tuwe miongoni mwa Mutaqeen (Wenye haki) tunapomruhusu yule Nabii aliye kama Musa, Masihi Isa, kutuongoza. Mwenyezi Mungu na akuwezeshe kuwa miongoni mwao ndiyo dua yangu inayotolewa kwa unyenyekevu leo hii.

## ‘Acheni Dhambi Zilizo Dhahiri na Zilizofichikana’ …

Somo letu hili linahusu Sheria ya Mwenyezi Mungu , - “Sharia ya Mwenyezi Mungu” – (Amri Kumi). Siku hizi watu husema kwamba Mwenyezi Mungu hana Sheria yo yote! Hata kutoka miongoni mwa waumini wamo wengi wasemao kwamba Sheria ya Mwenyezi Mungu, (kama ilivyoandikwa katika zile Amri Kumi) haiwafungi tena wanadamu leo. Je, ni kweli wanadamu wanaweza kuishi pasipo sheria zo zote?

### *Taifa Lisilokuwa na Sheria…*

Hebu na tuseme taifa fulani linachagua kufutilia mbali sheria zote. Kila mtu anakuwa huru kuchagua kile akitakacho. Kwa mfano, je, tungeweza kuona picha ya taifa lisilokuwa na sheria za usalama barabarani? Au hata vibaya zaidi, liwaondoe maafisa wote wa polisi wasifanye kazi zao za kusimamia sheria? Je, jambo hilo lisingeleta machafuko mabaya mno? Hakuna cho chote ambacho kingekuwa salama, maisha yangegeuka na kuwa matukio ya kuogofya sana. Wezi wangetwaa kile kilicho mali ya mwingine bila kujali maisha yake. Hakika maisha kama hayo yasingeingia mawazoni. Lakini, kwa sababu fulani watu wanajisikia kwamba ile Sheria ya Mwenyezi Mungu ya Amri Kumi haiwafungi wanadamu tena! Hebu fikiria mtu akisema, ‘Mwenyezi Mungu hajali mimi ninapokuwa na miungu mingine’, au ‘ni sawa tu kuiba’, au kwamba ni sawa kusema uongo kwa jirani yako au hata vibaya zaidi kupora mke wake au mali zake alizo nazo. Jumuia kama hiyo kwa hakika ingetoweka upesi.

Rafiki zangu, je, imepata kuwazukia wanadamu kwamba sababu ya ulimwengu huu kuwa na hali ngumu kama hii ni kwa kuwa watu wengi mno wameiweka kando Sheria ya Mwenyezi Mungu ya Amri Kumi (Sharia ya Mwenyezi Mungu) kama inavyopatikana katika Taurati, Kutoka 20. Katika Sura 2:93 twakumbushwa juu ya Sheria ile iliyotolewa.

002:093 ‘Na (kumbukeni habari hii kadhalika) Tulipochukua ahadi yenu (wazee wenu) na tukauinua mlima juu yenu (tukakwambieni): “Kamateni kwa nguvu haya tuliyokupeni na sikilizeni (hiyo Sheria)...” Sura 002:093 Al Baqarah

Je, Nabii huyu Mstahiki angeweza kuwaambia wasomaji wake ‘kamateni kwa nguvu haya tuliyokupeni na sikili-

zeni (hiyo Sheria)’, yaani, (Amri Kumi), kama yeye mwenyewe alikuwa haikubali ile Sheria kwa moyo wote? Je, isingefikiriwa kuwa ni kufuru kusema ‘kamateni kwa nguvu ile Sheria’, na huku yeye mwenyewe angekuwa anaihalifu Sheria Takatifu ya Mwenyezi Mungu katika maisha yake? Je, huu si wakati wa sisi wenyewe kuwa wakweli na kukubali kwamba vema, hapa ndivyo isemavyo kuhusiana na Sheria ya Mwenyezi Mungu! Katika Kurani Tukufu, twaambiwa kuacha dhambi zilizo dhahiri na zilizofichikana.

006:120 ‘Na acheni dhambi zilizo dhahiri na zilizofichikana. Hakika wale wanaochuma dhambi watalipwa yale waliyokuwa “wakiyachuma”’. Sura 006:120 Al An-am

Hapo zamani, watu wale wa kale kutoka Mashariki, walitambua fika maana ya ‘kuacha chambi.’ Watu hao wacha-Mungu walitambulikana katika Taurati, (Vitabu Vitakatifu) Ayubu 1:1 hunena habari za mtu mmoja aliyeitwa ‘Ayubu’. “Palikuwa na mtu katika nchi ya Usi, jina lake alikuwa akiitwa Ayubu; mtu huyo alikuwa mkamilifu na mwelekevu, ni mmoja aliyemcha [Mwenyezi Mungu, na kuepukana na uovu.” Ayubu 1:1 (Maandiko ya Biblia). Anatambuliwa na Mwenyezi Mungu kuwa “mtu huyo alikuwa ni mkuu sana kuliko watu wote wa upande wa mashariki’ Ayubu 1:3. Angewezaje mtu huyu kujua dhambi ni kitu gani, kama asingekuwa amefundishwa? Angewezaje kujua dhambi ni nini isipokuwa kama alikuwa ameijua Sheria ya Mwenyezi Mungu? Sisi twawezaje kujua dhambi ni nini isipokuwa kama tunaiangalia Sheria yake Mwenyezi Mungu? Dhambi yawezaje kufafanuliwa? Kwa hiyo Sheria [Amri Kumi] inahitajika ili sisi tupate kufahamu maana ya dhambi. (Injili) 1 Yohana 3:4 (TEV) “Kila mtu atendaye dhambi anavunja Sheria ya [Mwenyezi Mungu] Mungu, maana dhambi ni uvunjaji wa Sheria.”

Sheria hii imewekwa kwa ajili ya furaha ya mwanadamu. Kama watu mahali pote wangeitii, wangeijali, na kuiheshimu Sheria hii, furaha na amani iliyoje dunia yetu ingekuwa nayo. Mwenyezi Mungu angepewa heshima yake, uhai wa kila mtu ungelindwa kwa kicho. Jumuia leo ingekuwa tofauti sana, endapo wote wangeziangalia kwa heshima kubwa hizo Amri Kumi za Mwenyezi Mungu.

### *Kumi za Pekee za Mwenyezi Mungu…*

Endapo msomaji hazifahamu hizo Amri Kumi za Mwenyezi Mungu, basi, tunapenda kuiweka orodha hiyo ya sheria kumi fupi zilizotolewa kwa binadamu kutoka mbinguni. Tayari sisi tunajua kwamba Sheria hiyo ilitolewa zamani kabla ya kipindi cha Musa ilipoteremshwa juu ya vilele virefu vya Mlima Sinai. Maana Taurati yasema kwamba Ibrahimu yule ‘khalil wa Mwenyezi Mungu’ alizitii Amri za Mwenyezi Mungu.

(Taurati) Mwanzo 26:5 ‘Kwa sababu Ibrahimu alisikia sauti yangu, akayahifadhi maagizo yangu, na amri zangu, na hukumu zangu, na sheria zangu.’

Hapa twamwona mmoja kutoka zile nyakati za kale aliyekuwa mwaminifu kwa Mwenyezi Mungu, yaani, ambaye alizitunza na kuziheshimu Sheria za Mwenyezi Mungu. Je, sisi tusingefuata mfano wa Ibrahimu aliyekuwa ‘hanif’? Kisha kama ukumbusho, kwa kuwa mwanadamu alikuwa amesahau, Mwenyezi Mungu alirudia kuzitaja zile Amri kwa Musa juu ya Mlima Sinai. Kutilia uzito wa umuhimu wake moyoni mwa mwanadamu, Mwenyezi Mungu akaziandika Mwenyewe juu ya mbao za mawe.

Hapa chini zimeorodheshwa zile Amri Kumi kama zipatikanavyo katika: (Taurati) Kutoka 20:1-17.


“Mungu akanena maneno haya yote akasema, Mimi ni BWANA, Mungu wako, niliyekutoa katika nchi ya Misri, katika nyumba ya utumwa.

1. Usiwe na miungu mingine ila mimi.

2. Usijifanyie sanamu ya kuchonga, wala mfano wa kitu cho chote kilicho juu mbinguni, wala kilicho chini duniani, wala kilicho majini chini ya dunia. Usivisujudie wala kuvitumikia; kwa kuwa mimi, BWANA, Mungu wako, ni Mungu mwenye wivu; nawapatiliza wana maovu ya baba zao, hata kizazi cha tatu na cha nne cha wanichukiao, nami nawarehemu maelfu elfu wanipendao, na kuzishika amri zangu.

3. Usilitaje bure jina la BWANA, Mungu wako, maana BWANA hatamhesabia kuwa hana hatia mtu alitajaye jina lake bure.

4. Ikumbuke siku ya Sabato uitakase. Siku sita fanya kazi, utende mambo yako yote; lakini siku ya saba ni Sabato ya BWANA, Mungu wako, siku hiyo usifanye kazi yo yote, wewe, wala mwana wako, wala binti yako, wala mtumwa wako, wala mjakazi wako, wala mnyama wako wa kufuga, wala mgeni aliye ndani ya malango yako. Maana, kwa siku sita BWANA alifanya mbingu, na nchi, na bahari, na vyote vilivyomo, akastarehe siku ya saba; kwa hiyo




Miaka 2300, kwa mujibu wa unabii wa Danieli, ilikuwa “tangu kuwekwa amri ya kutengeneza na kuujenga upya Yerusalemu,’ hadi kufikia wakati ule wa patakatifu patakapotakaswa.

**457 K.K. –** Artashasta, Mfalme wa Uajemi, aliamuru kutenenezwa na kujengwa upya Yerusalemu (Danieli 0:24, Ezra 6:1,6-12). Huu ndio mwanzo wa miaka ile 2300.

**408 K.K. –** Kujengwa upya na kutengenezwa Yerusalemu kulikamilika katika kipindi cha kwanza cha miaka 49 ya unabii wa muda mrefu wa Danieli. Kazi ilikwisha mwaka 408 K.K. (Danieli 9:25).

**27 B.K. –** Yesu, alipakwa mafuta na Roho Mtakatifu wakati wa ubatizo wake, akaanza kuhubiri na kufundisha. Angalia Mathayho 3:16; Matendo 10:38. Kuanzia mwaka 457 K.K. hadi kufika kwa Kristo, “mpakwa mafuta,” ni miaka 483.

**31 B.K. –** Masihi “atakatiliwa mbali katikati ya juma,” 31 B.K., baada ya miaka mitatu na nusu ya utume wake mzuri. Angalia Danieli 9:27; Mathayo 27:50-51. Miaka mitatu na nusu iliyobaki ya juma lile la sabini inatufikisha mwisho wa kipindi cha miaka mia nne na tisini waliyopewa Wayahudi.

**34 B.K. –** Stefano apigwa mawe. Tangu wakati ule injili ilihubiriwa kwa Mataifa. Angalia Dan.9:24; Matendo 7:54-58:8:1.

BWANA akaibarikia siku ya Sabato akaitakasa.

5. Waheshimu baba yako na mama yako; siku zako zipate kuwa nyingi katika nchi upewayo na BWANA, Mungu wako.

6. Usiue.

7. Usizini.

8. Usiibe.

9. Usimshuhudie jirani yako uongo.

10. Usitamani nyumba ya jirani yako, usimtamani mke wa jirani yako; wala mtumwa wake, wala mjakazi wake, wala ng’ombe wake, wala punda wake, wala cho chote alicho nacho jirani yako.

Hivyo ndivyo zinavyofikia mwisho wake hizo sheria fupi kumi za Mwenyezi Mungu, ambazo zimeorodheshwa pia katika (Taurati) Kumbukumbu la Torati 5:6-21. Pia zimeorodheshwa katika sehemu mbalimbali za Injili.

## *Msamaha kutoka kwa Mwenyezi Mungu…*


Lakini swali hili mara kwa mara laweza kuwa mioyoni mwetu na katika akili zetu, ‘je, kunatokea nini mtu akitenda dhambi’? Je, kwa Mwenyezi Mungu kuna msamaha? Mtu ye yote akitenda dhambi, na kuomba msamaha, Mwenyezi Mungu ameahidi kusamehe. Lakini, hatuna budi kumwomba, na pia kuwa tayari kutubu na kuachana na maovu. Mwenyezi Mungu atatupa sisi toba, atatupa moyo unaohuzunika hadi kufikia mahali ambapo hatutaki tena kujishughulisha na dhambi. Zingatia maneno haya kutoka katika Injili … Matendo 5:31 “Mtu huyo [Masihi Isa] [Mwenyezi] Mungu amemtukuza kwa mkono wake wa kuume, awe Mkuu na Mwokozi [akfida], awape … toba na msamaha wa dhambi.” Ni kupitia kwake Masihi Isa aliyeteremshwa na Mwenyezi Mungu tunapata toba na msamaha wa dhambi. Isa akawa ukombozi [fidia] kwa ajili ya dhambi kwa ajili ya taifa la kibinadamu. Yeye ndiye tunu kubwa kwetu kutoka kwa Mwenyezi Mungu! Hebu na tuishikilie tunu hiyo, wala tusimkatae yeye aliyeteremshwa kuja kwetu! Yatupasa tusikose kulielewa suala hili! Ni kwa njia ya Masihi Isa sisi tunapewa msamaha! Mpokeeni Yeye!

## *Masihi Isa anatupa uwezo…*

Twamgeukia tena yule mtu wa kale aliyetoka Mashariki ambaye kama zisemavyo kumbukumbu … ali“epukana na uovu”. Ayubu 1:1 (Taurati). Aliwezaje kufanya vile? Ni kwa jinsi gani mtu ye yote anaweza kuepukana na uovu? Je, mwanadamu anao uwezo ndani yake mwenyewe wa kufanya vile? Je, mtu kwa nguvu zake mwenyewe anaweza kupigana na kumshinda Ibilisi (Shetani)? Taurati inaandika yafuatayo: Yeremia 17:5 “BWANA asema hivi, Amelaaniwa mtu yule amtegemeaye mwanadamu [kuwa nguvu zake], amfanyaye mwanadamu kuwa kinga yake na moyoni mwake amemwacha BWANA.” Kwa mwanadamu ni kushindwa tu, hakuna tumaini katika kujitegemea wenyewe au mtu mwingine kutuokoa kutoka katika hali yetu ya kuanguka [dhambini]. Twaweza tu kuwa na tumaini tunapomwangalia Mwenyezi Mungu na Yeye aliyeteremshwa kuja hapa chini kama msaidizi wetu, yaani, Masihi Isa!

(Injili) Yohana 1:12 “Bali wote waliompokea [Masihi Isa] aliwapa uwezo wa kufanyika watoto wa Mungu, ndio wale waliaminio jina lake.” Je, si huo uwezo ambao sisi sote tunauhitaji? Uwezo wa kuyashinda maisha yetu yenye dhambi! Uwezo wa kufanya mambo yaliyo ya haki! Hebu sikiliza Ewe mpendwa rafiki yake Mwenyezi Mungu, ni kwa njia ya Masihi Isa tunapokea uwezo huo utokao kwa Mwenyezi Mungu. (Injili) 1 Yohana 1:9 “Tukiziungama dhambi zetu, Yeye ni mwaminifu na wa haki hata atuondolee dhambi zetu, na kutusafisha na udhalimu wote.”

011:052 “Na enyi watu wangu! Ombeni msamaha kwa Mola wenu (kwa mabaya yenu yaliyopita), kisha mtubie kwake (kwa kufanya mema sasa na kuacha mabaya), atakuleteeni mawingu yateremshayo mvua tele, na atakuzidishieni nguvu juu ya nguvu zenu (mlizonazo). Wala msikengeuke kuwa waovu.” Sura 011:052 Hud




Kuanzia mwaka 457 K.K. hadi "majira ya Mataifa yatakapotimia," ni miaka 490 au majuma sabini.

**1. 570 B.K. –** Muhammad Azaliwa Ufu. 9:1(Nyota).

**2. 632 B.K. –** Muhammad Alikufa.

**3. 622 B.K. -Hadi Julai 27, 1449 –** Baragumu Ya 5 – Ole Wa 1, Ufu.9:1-12 Uislamu.

**4. Julai 27, 1449 Hadi Agosti 11, 1840 –** Baragumu Ya 6 – Ole Wa 2, Ufu.9:13 - 11:14 Uislamu.

**5. Agosti 11, 1840 Hadi Marejeo Ya Kristo –** Baragumu Ya 7 – Ole Wa 3, Ufu.11:15-19 Uislamu.

**6. Wana Wa Mashariki -** Uislamu Watumika Kama Kiboko Dhidi Ya Ukristo Ulioasi.

**1844 B.K. –** Ujumbe wa Malaika Watatu wa Ufunuo 14:6-12 kutangazwa ulimwenguni kote kabla tu ya kuja kwake Kristo mara ya pili.

**1844 B.K. –** Mwisho wa miaka 2300. Kutakaswa kwa Patakatifu pa Mbinguni katika saa ya hukumu ya Mungu. Angalia Dan.8:14; Ufunuo 14:7.

**7. JAN. 1984 –** Rais Ronald Reagan Amteua Balozi Kwenda Vatikani. Amerika Ya Kiprotestanti Yatimiza Sehemuyake Kama "Nabii Wa Uongo" Wa Ufunuo16:13-16; 13:11-17. Amerika Imefanya Mapatano Ya Siri Ya Danieli 11:40.

## "Jinsi Ayubu alivyopoteza afya yake na utajiri wake"

### *Mafumbo Mawili!*

Pengine wewe unakijua kisa cha Ayubu na jinsi alivyokuwa miongoni mwa watu mashuhuri sana wa Mashariki katika zama zile za kale. Lakini alipitia kilele cha kutisha cha ugonjwa na kupoteza utajiri wake pamoja na sehemu kubwa ya familia yake na hatimaye afya yake iliathirika vibaya sana (Sad 41). Ayubu alipata mateso makali sana. Je, ni nani alihusika na hayo? Kupata jibu kwa kisa

hiki hutatua mafumbo mawili maalumu…

Je, ni nani aliyemletea Ayubu maumivu makali kama yale, huzuni na hasara ile? Mtu mbaya sana kama huyo angewezaje kuumbwa? Kwa somo hili na somo lo lote jingine tunahitaji sana kutoa dua zetu faraghani maana Mwenyezi Mungu kwa kweli atawaongoza na kuwaelekeza wale wamtafutao kwa dhati. Mwenyezi Mungu ambaye mara kwa mara husamehe na amejaa fadhili (Al-Buruj 14) awe karibu nawe mpendwa msomaji.

Je, hivi Mwenyezi Mungu ambaye ni Mwenye kuneemesha neema kubwa kubwa na Mwenye kuneemesha neema ndogo ndogo (Al Fatihah 1) angeweza kumwumba Ibilisi (Shetani)? Je, yule Aliye Mtakatifu, aliye chimbuko la Amani na Ukamilifu, Mkuu kuliko wote, Aliyetukuzwa tena ambaye ni Mlinzi, na Mhifadhi wa Usalama (Al-Hashr 23), angeweza kuumba dhambi na Shetani yule mwovu? Je, yule aliye na majina mazuri sana (Al Aaraf 180) anaweza kujihusisha kuumba kitu kibaya sana kama dhambi na uovu?

Au lilikuwa ni chaguo la Ibilisi alilofanya, ambalo lilimfanya kuwa Shetani yule mwovu, na Mwenyezi Mungu alimruhusu tu kuwa na uhuru wa kuchagua?

Mwenyezi Mungu hahusiki na kuwako kwake dhambi, ila yeye anayo tiba yake. Si Mwenyezi Mungu aliyefanya dhambi iweko, hata ingawa wengine wanadhani kwamba Mwenyezi Mungu ambaye ni Mtakatifu, Mwenye haki na aliye safi kabisa angeweza kuumba Uovu! La, hasha, tusiwaze mawazo kama hayo... kitu kama hicho kisingeingia mawazoni mwetu kuwa Mwenyezi Mungu anahusika na kuwako kwa uovu.

### *Ilivyotokea mwanzoni!*

Haya basi, ilitokeaje? Kwa maana wote wanaweza kuona dhahiri ya kwamba kweli kuna ufisadi wa kutisha duniani na uovu kila mahali tuangaliako. Vitabu Vitakatifu vinatupa ujuzi juu ya jinsi Ibilisi alivyotokea. Katika Taurati inatuambia sisi kwamba toka mwanzo, mtu huyo, ambaye sasa anaitwa Shetani alikuwa na jina la Lusifa (Taurati Isaya 14:12). Lusifa maana yake "Mchukuzi wa Nuru". Wakati mmoja alikuwa malaika aliyetukuzwa ambaye alikuwa katika mlima wa Mwenyezi Mungu. (Taurati Ezekieli 28:14-15) "Wewe ulikuwa kerubi mwenye kutiwa mafuta afunikaye; nami [Mwenyezi Mungu] nalikuweka hata ukawa juu ya mlima mtakatifu wa Mungu, umetembea huko na huko kati ya mawe ya moto. Ulikuwa mkamilifu katika njia zako tangu siku ile ulipoumbwa, hata uovu ulipoonekana ndani yako."

Mwenyezi Mungu alimwumba Lusifa akiwa safi, mtakatifu na kiumbe mzuri sana. Taratibu wakati ulipopita, Lusifa akaanza kujiangalia mwenyewe na kujikweza mwenyewe badala ya Muumbaji. Aliutamani uzuri wake na kujifikiria sana kuliko alivyopaswa kufikiri. Mawazo kama hayo yalimfikisha mahali ambapo huyo Lusifa alitaka kukipindua kiti cha enzi cha Mwenyezi Mungu. (Taurati Isaya 14:12-14) "Jinsi ulivyoanguka kutoka mbinguni, Ewe nyota ya alfajiri (Lusifa), mwana wa asubuhi! Jinsi ulivyokatwa kabisa, Ewe uliyewaangusha mataifa! Nawe ulisema moyoni mwako, Nitapanda mpaka mbinguni, Nitakiinua kiti changu juu kuliko nyota za Mungu; Nami nitaketi juu ya mlima wa mkutano, katika pande za mwisho za kaskazini. Nitapaa kuliko vimo vya mawingu, Nitafanana na yeye Aliye juu."

Hasa hasa yeye alikuwa hapatani kabisa na Masihi Isa aliyekuwa karibu sana na Mwenyezi Mungu (Aali Imran 45). Lusifa, yule malaika

afunikaye, baada ya muda mwingi kupita aliendeleza chuki dhidi ya Masihi Isa, ambayo ilijitokeza katika maasi ya wazi. Lusifa hakuwa katika baraza la wale Watawala Wakuu walipojadili mambo kati yao (Sad 69). Yaonekana ya kwamba wale Watawala Wakuu walikuwa wakiongea juu ya uumbaji wa mwanadamu, na Lusifa hakuwamo katika hilo Baraza Kuu, yeye alikuwa tu ni kiumbe aliyeumbwa. Viumbe walioumbwa hawakuruhusiwa kuingia katika baraza hilo. Ni jambo la kusikitisha, lakini ni la kweli, Lusifa Mchukuzi wa Nuru, alizitumia vibaya fadhila takatifu alizopewa na kuzipotoa njia zake kutokana na mawazo yake machafu. Akawa hana furaha pamoja na cheo chake kitukufu alichokuwa nacho akiwa karibu na kiti cha enzi cha Mwenyezi Mungu, kisha ubinafsi ukatia mizizi ndani yake.

Hilo likasababisha maasi makubwa kule Mbinguni, Lusifa alipoeleza kutoridhika kwake miongoni mwa malaika wengi. Chuki hiyo na mawazo machafu, vikawa kama ugonjwa unaoogopwa uambukizao, na wengi wa wale waliomsikiliza walichagua kuwa upande wa Lusifa. Nao pia wakawa wamedanganywa na kupotoshwa, kutokana na hila zake Lusifa. Watawala wale Wakuu waliwaeleza wazi malaika kwamba endapo wangesisitiza kuyafuata mawazo hayo potofu ya Lusifa, basi, ingewalazimu kuondoka Mbinguni.

### *Vita Mbinguni?*

Naam, hatimaye pakawa na vita mbinguni! Injili Ufunuo 12:7-9 "Kulikuwa na vita mbinguni; Mikaeli [Masihi Isa] na malaika zake wakapigana na yule joka [Shetani]; yule joka naye akapigana nao pamoja na malaika zake; nao hawakushinda, wala mahali pao hapakuonekana tena mbinguni. Yule joka akatupwa,yule mkubwa, nyoka wa zamani, aitwaye Ibilisi na Shetani, audanganyaye ulimwengu wote; akatupwa hata nchi, na malaika zake wakatupwa pamoja naye." Masihi

## "Upendo wa Mwenyezi Mungu kwa Waislamu"

Isa akasema… "Nilimwona Shetani, akianguka kutoka mbinguni kama umeme." Injili Luka 10:18. Wakati mmoja alikuwa kiumbe aliyetukuzwa, akichukua nuru baadaye anaanguka. Je, twaweza kuiona picha kama hiyo, Mbinguni mahali pa amani na utulivu sasa panageuka na kuwa mandhari ya vita?

Shetani alihoji mapenzi matakatifu ya Mwenyezi Mungu, na kazi yake ya kwanza kabisa ilikuwa ni kuivunja sheria ya Mwenyezi Mungu [zile Amri Kumi]. Baadaye akaja kwa Adamu na Hawa katika bustani ya Edeni na kwa njia ya majaribu yake, aliwafanya pia kutoliamini neno lake Mwenyezi Mungu na jambo hilo likawafanya wazivunje amri. Ulikuwa ni mpango wa Shetani kupigana vita na Mungu wa mbinguni na kuzipiga vita sheria zake Takatifu kule mbinguni na kisha hapa duniani. Mwenyezi Mungu anayo katiba yake na sheria ili kuwatawala wale aliowaumba. Lingekuwa kosa la kutisha kujiunga upande wa Shetani na kukutwa upande mbaya, ukipigana na serikali ya Mbinguni na sheria zake Takatifu na za haki, yaani, zile Amri Kumi.

Baada ya Shetani kutupwa, aliweka makao yake makuu hapa duniani. Anaendelea kudanganya kama alivyofanya kule mbinguni. Ila sasa uwezo wake wa kudanganya ni mkubwa zaidi. Yeye bado yuko nyuma ya uhalifu, vita, chuki, na umwagaji damu tunaouona duniani leo. Anaendeleza kupanda mbegu za uovu, uhalifu, na chuki juu ya wanadamu, lakini Mwenyezi Mungu katika rehema zake nyingi na huruma zake, hatuachi bila kutupa msaada wake. Mwenyezi Mungu Bwana wa ile kweli bado anatupa Roho wa Mwenyezi Mungu (Roho Mtakatifu) kuwatia nguvu wale waaminio (An Nahl 102). Leo hii sisi twaweza kudai ahadi isemayo kwamba wote wanaokuja kwa Mwenyezi Mungu kwa njia ya mjumbe wake aliyemteua Masihi Isa wanaweza pia kujazwa na Roho wa Mwenyezi Mungu (Roho Mtakatifu) na kuweza kupambana na adui huyu mwenye hila nyingi (Shetani)… "kwa maana [mimi Mwenyezi Mungu] nitateta (nitapambana) na yeye atetaye nawe…" Taurati Isaya 49:25

### *Ni nani aliyemsumbua Ayubu na kumletea huzuni kubwa?*

Sasa ili kulijibu swali letu lile la kwanza kuanzia mwanzo wa mazungumzo yetu haya…nani aliyeleta mateso na uovu katika maisha ya Ayubu? Taurati Ayubu 1:8 "Kisha BWANA akamwuliza Shetani, Je! umemwangalia huyo mtumishi wangu Ayubu? Kwa kuwa hapana mmoja aliye kama yeye duniani, mtu mkamilifu na uelekevu, mwenye kumcha Mungu na kuepukana na uovu." Alikuwa si mwingine zaidi ya yule Shetani,yule aliyeanguka kutoka mbinguni. Kisa hicho kinaendelea… Taurati Ayubu 1:9-21 "Ndipo Shetani akamjibu BWANA, na kusema, Je! huyo Ayubu yuamcha BWANA bure? Wewe hukumzingira kwa ukigo pande zote, pamoja na nyumba yake, na vitu vyote alivyo navyo? Kazi za mikono yake umezibarikia, nayo mali yake imeongezeka katika nchi. Lakini nyosha mkono wako sasa, uyaguse hayo yote aliyo nayo, naye atakukufuru mbele za uso wako. BWANA akamwambia Shetani, Tazama, yote aliyo nayo yamo katika uwezo wako; lakini usinyoshe mkono wako juu yake yeye mwenyewe. Basi Shetani akatoka mbele za uso wa BWANA. Ilitukia siku moja hao wanawe na binti zake walipokuwa wakila na kunywa divai katika nyumba ya ndugu yao mkubwa, mjumbe akamfikilia Ayubu na kumwambia, Hao ng'ombe walikuwa wakilima, na punda walikuwa wakilisha karibu nao; mara Waseba wakawashambulia, wakawachukua wakaenda nao; naam, wamewaua watumishi kwa makali ya upanga, nami peke yangu nimepona, mimi tu, kukuletea habari. Huyo alipokuwa akali akinena, akatokea na mwingine, na kusema, Moto wa Mungu umeanguka kutoka mbinguni na kuwateketeza kondoo, na wale watumishi, na kuwaangamiza; mimi peke yangu nimepona, mimi tu, kukuletea habari. Huyo alipokuwa akali akinena, akatokea na mwingine, na kusema, Wakaldayo walifanya vikosi vitatu, wakawaangukia ngamia, wakaenda nao, naam, wamewaua wale watumishi kwa makali ya upanga; mimi peke yangu nimepona, mimi tu, kukuletea habari. Huyo alipokuwa akali akinena, akatokea na mwingine, na kusema, Wanao na binti zako walikuwa wakila na kunywa divai katika nyumba ya ndugu yao mkubwa; mara, tazama, upepo wenye nguvu ukatoka pande za jangwani, ukaipiga hiyo nyumba pembe zake nne, nayo ikawaangukia hao vijana, nao wamekufa; na mimi peke yangu nimepona, mimi tu, kukuletea habari. Ndipo Ayubu akainuka, akalirarua joho lake, kisha akanyoa kichwa chake, na kuanguka na nchi, na kusujudia; akasema, Mimi nalitoka tumboni mwa mama yangu, nili uchi, nami nitarudi tena huko uchi vilevile; BWANA alitoa, na BWANA ametwaa; jina la BWANA na libarikiwe." Ni Shetani anayewatesa wote wanaochagua kumfuata Mwenyezi Mungu, lakini uwezo wa Shetani una mipaka yake. Hawezi kutugusa zaidi ya vile Mwenyezi Mungu anavyomruhusu. Siku moja inayokuja upesi uwezo wa Shetani utavunjiliwa mbali. Basi wewe sasa unalijua lile fumbo linalohusu Shetani alivyotokea. Hebu na ukae karibu na Mwenyezi Mungu na Wale anaowatuma kwetu sisi… Roho Mtakatifu (Ruh) na Masihi Isa. Mwenyezi Mungu na akujalie Amani yake ya milele.

**Kwa maelezo zaidi:**

**www.salahallah.com** **www.allahshanif.com** **www.swahilitruth.com**